# KAULI YA MHESHIMIWA WAZIRI



**Mheshimiwa Dkt. Riziki Pembe Juma**
Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo

Kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Tume ya Utangazaji Zanzibar (TUZ) kwa kuanzisha jarida hili lenye lengo la kufikisha ujumbe moja kwa moja kwa jamii kutokana na shughuli wanazozifanya.

Hatua hii ni muhimu katika kipindi hiki ikizingatiwa kuwa kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano kumewezesha kuwepo kwa ongezeko la wadau ambao wanahitaji kufahamu kwa kina juu ya TUZ na majukumu yake.

Ni fursa muhimu pia kwa TUZ kujitangaza kwa wadau wake juu ya shughuli inazozifanya na kuwaweka karibu ili waweze kutoa maoni na mapendekezo ya kufanikisha kwa ufanisi majukumu hayo.

Bila shaka, TUZ ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Na 7 ya mwaka 1997 ina wajibu wa kuelimisha umma na kuupa habari juu ya shughuli za utangazaji ambazo inazisimamia kwa mujibu wa Sheria hiyo.

TUZ pia ina wajibu wa kuhakikisha kuwa utamaduni, mila na silka za Zanzibar zinalindwa huku kukiwa na kasi ya kukua kwa matumizi ya vyombo vya utangazaji hapa Zanzibar.

Nina hakika tunaelewa kwamba utamaduni ndio muhimili mkuu katika kuendeleza nchi, na kwamba utamaduni wa taifa unaposhindwa kulindwa taifa linaweza kuingi katika mashaka makubwa.

Kukua kwa sayansi na teknolojia ni mfano hai wa mabadiliko ya kasi katika kila nyanja ya jamii. Utamaduni ukiwa umeguswa zaidi kutokana na urahisi wa mawasiliano.

Kuongezeka kwa utaalamu kumeongeza fursa ya wanajamii kutengeneza maudhui mbali mbali. Mengine ni mazuri na yenye tija kwa jamii, lakini mengine yamekuwa yakiandaliwa maalum kwa kuweza kusambaza kashfa kwa wengine.

Baadhi ya maudhui haya huchafua hadhi za watu na kuingilia faragha zao, na kuharibu taswira ya nchi.

Nchi nyingi duniani sasa zimekumbwa na taharuki na nyingi zimekuwa zikipinduliwa kutokana na maudhui wakati mwengine yasiyokuwa sahihi ambayo yamekuwa yakisambazwa mitandaoni.

Kwa kuwa waandaaji wa maudhui hayo wamekuwa hawaonekani, wengi wamekuwa wakiyaamini, licha ya kwamba mengi yao hayana ukweli.

Maelezo yangu haya yanaashiria kuwa ipo haja kubwa kwa TUZ kuendelea kushika kani katika kutekeleza majukumu yake ya msingi ambayo yanalenga kuweka utaratibu mzuri wa kuendesha na kudhibiti shughuli za utangazaji na urushaji wa maudhui na hasa mtandaoni.

Natambua kwamba licha ya kuwa TUZ imekuwa ikifanya kazi katika mazingira magumu, lakini juhudi ya kazi zao imekuwa chachu ya mafanikio hapa Zanzibar.

Hatua hii tunaweza kuipima kutokana na kuongezeka kwa idadi ya vituo vya utangazaji hapa Zanzibar, na kuendelea kuimarika kwa sekta ya utangazaji kunakotokana na kazi kubwa ya kufuatilia maudhui na kuvikagua vituo vya utangazaji.

Mara kadhaa tumeshuhudia TUZ ikifanya ziara ya kuvitembelea vituo mbali mbali vya utangazaji na kuvichukulia hatua kwa mujibu wa sheria vile ambavyo vinabainika kuwa na kasoro za kiutendaji.

Tume ya Utangazaji Zanzibar ni muhimili ni wajibu kwa kila mdau kuipatia kila aina ya msaada ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Nikiwa msimamizi mkuu wa Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, naungana na wenzangu wote katika wizara hii kuhakikisha ustawi na mustakbali mwema wa TUZ katika shughuli zao za kila siku.

Tunawapongeza viongozi na watendaji wa TUZ kwa kufikiria umuhimu wa kuanzisha jukwaa hili la mawasiliano na wadau. Nasi kama Wizara tupo tayari kuwaunga mkono katika hatua zote zitazohitajika ili jarida hili lidumu kwa miaka mingi.

Tunaimani kuwa sauti za wananchi ambazo zitasikika kupitia jarida hili si tu zitaihusu Tume na mambo inayoyasimamia, bali pia Wizara kwa ujumla wake ikizingatiwa kuwa yenyewe ndio mlezi wa taasisi zote zilizopo chini ya Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo.

Tunawatakia usomaji mwema wa jarida hili na utekelezaji bora wa majukumu ya utangazaji tukiamini kuwa ujumbe utaopatikana utastawishi sekta ya utangazaji na maendeleo ya mawasiliano kwa ujumla.

Mhe. Riziki Pembe Juma
Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo
Zanzibar

# TAHARIRI



**Hiji Dadi Shajak**
Katibu Mtendaji, Tume ya Utangazaji Zanzibar

# Tutumie fursa ya kujielimisha kupitia jarida jipya la TUZ

Kwa mara ya kwanza katika historia, Tume ya Utangazaji Zanzibar (TUZ) imeanzisha jarida liitwalo Sauti ya Tume.

Jarida hili linalenga kukupa taarifa juu ya mambo mbali mbali yanayohusiana na utangazaji, maendeleo ya sekta ya utangazaji na taaluma ya masuala mbalimbali ya sheria na taratibu za utangazaji.

Jarida hili litakalokuwa likitoka kila robo mwaka litakuwa ni nyenzo na jukwaa la mawasiliano kati ya TUZ na wadau mbalimbali.

Kupitia jarida hili wadau wetu pia watapata fursa ya kutoa maoni na mapendekezo yatakayokuwa chachu ya kuimarisha shughuli za Tume na sekta ya utangazaji kwa ujumla.

Ni matarajio yetu kuwa kila atakaefuatilia jarida hili atajifunza mengi muhimu kuhusu sekta ya utangazaji.

Katika jarida hili la kwanza, tunakuletea makala zinazokupa uelewa juu ya Tume na shughuli zake kwa ujumla, umuhimu wa taaluma ya uanzishaji wa kituo cha utangazaji, kiwe redio au televisheni, na sheria zinazosimamia sekta ya utangazaji hapa Zanzibar.

Wadau wengi wamejitokeza kuanzisha vituo vya utangazaji, lakini kwa bahati mbaya wamekosa taaluma ya msingi ya kibiashara katika eneo hilo.

Matokeo yake ni kuwa wadau hao hujikuta wakiwa katika wakati mgumu kuendeleza shughuli zao kwa ufanisi kutokana na kukabiliwa na changamoto kadhaa za uendeshaji zikijimuisha ulipaji wa ada mbalimbali zinazodaiwa na vyombo vya usimamizi kama vile TUZ.

Jarida hili litaendelea kukujuvya haya na yale katika kufuatilia na kustawisha shughuli zinazohusu utangazaji ukiwa kama mdau wetu muhimu.

Toleo hili linakuja kukiwa na ongezeko kubwa la vituo vya utangazaji na hasa vinavyorusha maudhui mtandaoni.

Hii ni kwa sababu uwekezaji wa utangazaji mtandaoni umekuwa ni rahisi na unawezesha kufika eneo kubwa zaidi na kwa muda mfupi.

Ongezeko hilo linailazimisha Tume kuimarisha mikakati yake ya kufuatilia mitandao hiyo na kuona iwapo sheria kanuni na miongozo ya utangazaji inafuatwa.

Hivyo, ninawanasihi wadau wetu kuzingatia matakwa ya sheria katika kuendesha vituo vya utangazaji na kila mmoja achukue fursa ya kukumbusha mwengine juu ya haja ya kutii sheria.

Tunaamini kuwa hatua hii itasaidia kupunguza changamoto zinazojitokeza kwa waanzishaji wa vituo binafsi pamoja na TUZ ambayo ina jukumu la usimamizi.

Baada ya miaka 24 tangu kuanzishwa TUZ, na kukua kwa teknolojia ya utangazaji duniani, tunaendelea kujipima pale tunapotoka, tulipo sasa na tunapoelekea. Awamu ya nane inayoongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi inahimiza matumizi ya mtandao ya kidigitali katika kuimarisha uchumi, na yapo matarajio makubwa ya kuongezeka warushaji wa maudhui ya mtandaoni.

Nasi tutajitahidi kuendelea kuwashauri wadau njia bora za kutumia teknolojia katika uwekezaji wa utangazaji ili malengo na matarajio yaweze kufikiwa.

Wakati tukiendelea kuiongoza Tume kwa matarajio, tunajadili na kuzingatia nini tunapaswa kukifanya kwa changamoto zinazotukabili na kupanga mbinu bora za namna ya kukabiliana nazo katika siku zijazo.

Ofisi yetu inahitaji mabadiliko ambayo tunaamini ujio wake utasukumwa na michango muhimu ya wadau wake.

TUZ ipo tayari kushauriwa na kukosolewa na inaahidi kupokea ushauri na kujirekebisha ili kuimarisha shughuli zake.

Tunaamini kipindi hiki cha pili cha awamu ya nane kitakuwa na mabadiliko makubwa zaidi yaliyofanywa katika kuimarisha shughuli zetu katika kila eneo.

Karibuni sana katika jukwaa la utangazaji!

# Ijue Tume ya Utangazaji Zanzibar (TUZ)

ZANZIBAR BROADCASTING COMMISSION

TUME YA UTANGAZAJI ZANZIBAR

Utangazaji ndio njia ya mawasiliano inayofahamika zaidi na yenye nguvu duniani.

Katika sehemu nyingi ambazo watu wake wana kiwango kidogo cha maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano, ufikiaji pekee wa habari na taarifa ni kwa njia ya mdomo, au redio.

Kati ya hizo mbili, redio ndiyo yenye uwezo zaidi. Katika maeneo yaliyoendelea kiasi, televisheni imechukua nafasi ya redio kama chanzo kikuu na kinachoaminika zaidi cha habari.

Kwa upande wa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) iliona kuna haja ya kutanua wigo wa upatikanaji wa habari kwa kuhusisha sekta binafsi katika uanzishaji na uendeshaji wa huduma za utangazaji.

Ikiwa na lengo la kufanikisha haja ya kukuza uhuru wa habari kwa matumizi ya redio na televisheni, SMZ iliunda Tume ya Utangazaji Zanzibar (TUZ) ili kusimamia vituo vya utangazaji.

Tume, ikiwa ni Taasisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyo chini ya Wizara ya Habari, Sanaa Utamaduni, na Michezo, imeundwa kwa Sheria ya Tume ya Utangazaji nambari 7 ya Mwaka 1997 na kuanza kazi yake rasmi tarehe 26 Machi 2002 baada ya kuteuliwa rasmi Mwenyekiti na Katibu Mtendaji wa kwanza wa Tume hiyo.

Dhamira yake kuu ni *"kutoa huduma bora na za kuaminika za utangazaji kwa umma kupitia kuwezesha viwango vya juu na uvumbuzi"*. Dhamira hiyo inaungwa mkono na kauli mbiu isemayo *"Pata taarifa kwa ustadi"*.

Kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utangazaji, Tume inaundwa na Mwenyekiti ambaye anateuliwa na Rais na wajumbe wasiozidi sita.

Kati ya hao, wajumbe wasiozidi wanne wanateuliwa na Mhe. Waziri anaehusika na Habari na mjumbe mmoja kutoka ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, yupo Katibu Mtendaji anaeteuliwa na Rais ambaye pia ni Katibu wa Tume na kiongozi wa sekretarieti.

**Majukumu ya TUZ**

Kwa kuzingatia umuhimu wake kama ilivyotajwa hapo juu, Sheria ya Utangazaji, kifungu nambari 7 kinataja majukumu ya Tume ya Utangazaji yakiwemo:

a) Kutoa leseni za Utangazaji.
b) Kuongoza na kusimamia shughuli zote za utangazaji nchini, ikiwemo matangazo ya redio na Televisheni.
c) Kuweka daftari la vituo vya utangazaji vilivyosajiliwa, iwe vituo vya redio na TV, wafanyabiashara wa vifaa vya utangazaji, waagiziaji na mafundi wanaofunga na kutengeneza vifaa vya utangazaji.
d) Kupanga, kuweka viwango na kudhibiti matumizi ya mawimbi ya kutangazia (frequency spectrum), na kutoa mawimbi hayo katika hali ambayo itahakikisha yanatumika ipasavyo na kwa ufanisi.
e) Kulinda sera, usalama, mila na utamaduni wa Mzanzibari usiharibiwe.
f) Kukagua taasisi inayojishughulisha na biashara ya utangazaji.
g) Kutoa miongozo kuhusiana na biashara ya utangazaji kama vile itakavyoona inafaa.

**Umuhimu wa TUZ**

Vyombo vya habari vya utangazaji vinaweza kuathiri mawazo na tabia za watu kwa kiwango kikubwa, kwa mema na mabaya. Vituo vya utangazaji vinapaswa kusimamiwa ili kukuza utamaduni ikiwemo lugha asili ya Kiswahili.

Tume pia ina nafasi ya kusaidia kulinda heshima, taswira na hadhi ya wananchi mbele ya jamii kwa kuhakikisha kuwa hakuna kituo cha utangazaji kinachovunja heshima ya mtu au kuingilia faragha yake.

Tume inapaswa kuhakikisha kuwa mambo muhimu ya kitaifa yanapewa nafasi katika vituo vya utangazaji ili umma uweze

kufahamu masuala ya nchi, bila ya kujali kuwa kituo hicho ni cha serikali au mtu binafsi.

Kwa mfano, unapofika wakati wa uchaguzi, Tume ya Utangazaji huwataka watoa huduma kufuata miongozo maalum ya utangazaji wakati wa uchaguzi pamoja na kuhakikisha kuwa matangazo yanayohusu mchakato huo yanatolewa kwa usawa na bila ya upendeleo.

Usimamizi wa Tume unaonekana pia kunapotokea hali ya dharura ambapo kupitia Kanuni za Utangazaji taasisi hiyo hutoa miongozo ya jinsi ya kuripoti na kutangaza matukio hayo ili kuepusha taharuki.

Kila taaluma ina maadili yake, na utangazaji nao kama ni sehemu ya tasnia ya habari unasimamiwa na misingi mbalimbali.

Tume ya utangazaji inahakikisha kuwa vipengele vyote vinavyohusu maadili vinafanyiwa kazi ipasavyo ili matangazo yakidhi vigezo vya kitaaluma, na si tu utashi wa mtangazaji.

Hivyo, Tume inasimamia watoa huduma za utangazaji ili kuhakikisha viwango bora vya huduma, kufuatwa kwa maadili, na huduma zinazoendana na thamani ya fedha.

Tume pia inazingatia ukuzaji wa teknolojia ya utangazaji kwa kuanzisha njia mpya za usambazaji wa maudhui za kidijitali.

Kwa msingi huu, TUZ imesimamia kuanzishwa kwa vituo vipya vya redio na Televisheni nchini ambapo hadi sasa imefanikiwa kutoa jumla ya leseni 109 kwa vituo vya Utangazaji vya Unguja na Pemba zikiwemo 11 za Televisheni, 60 za maudhui ya mtandaoni, 32 za vituo vya redio na leseni sita za wasambazaji maudhui.

Ili kufanikisha jukumu lake ipasavyo na kwa kuzingatia kuwa teknolojia hivi sasa imekuwa, Tume imefunga mitambo ya kufuatilia maudhui ya utangazaji ili kuhakikisha vituo vya utangazaji vinafuata masharti yaliyowekwa.

Ufuatiliaji pia hufanywa kwa ziara za kawaida ambapo Tume hushauri juu ya njia bora ya kuweza kuimarisha shughuli za utangazaji baada ya kubainika changamoto za kiutendaji.

Kwa kuimarisha mahusiano na wadau hawa, Tume hufanya mikutano ya mara kwa mara ili kuelimishana pamoja na kubaini changamoto na maendeleo ya vituo vya utangazaji kadri siku zinavyosonga mbele.

**Nani anaongoza TUZ?**

Hivi sasa Tume inaongozwa na Katibu Mtendaji, Hiji Dadi Shajak ambae katika awamu hii ya uongozi ameweza kukabili changamoto kadhaa za kiutendaji zinazorudisha maendeleo ya Tume na kuwezesha mageuzi makubwa yanayoendelea kuonekana katika Tume hiyo siku hadi siku.

Aidha, katika usimamizi wa juu zaidi, Tume inaongozwa na Mwenyekiti wake, ambae kwa sasa ni Suleiman Ame Khamis. Akisaidiana na wajumbe wake, mwenyekiti ameweza kusimamia vyema ukuaji wa Taasisi hii kwa kuruhusu mabadiliko muhimu yanayohitajika ili Tume iendelee ikiwemo kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji matangazo na mifumo ya kufuatilia malipo ya huduma yanayofanywa na wadau.

Ofisi za TUZ zipo Kilimani Unguja, na kwa Pemba zipo Mkoroshoni, Chake Chake.

# Tume ya Utangazaji Zanzibar yajivunia mafanikio awamu ya nane



Na Asha Abdi Makame

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2002, Tume ya Utangazaji Zanzibar (TUZ) imekuwa ikirekodi mafanikio awamu baada ya awamu. Mafanikio hayo yameiwezesha Tume kuendelea kukua na kuimarika siku hadi siku huku ikitekeleza kwa ufanisi majukumu ya msingi iliyopangiwa.

Hata hivyo, katika uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nane, Tume imeweka alama muhimu za mafanikio zinazotokana na mipango thabiti ya serikali katika.

Miongoni mwa mafanikio hayo ni ufungaji wa mfumo na vifaa vya ufuatiliaji maudhui, ZBC TV kurushwa (kubebwa) na mitandao yote ya usambazaji wa maudhui nchini na kuongezeka kwa vituo vya utangazaji hapa Zanzibar.

**Vifaa na mfumo wa ufuatiliaji maudhui.**
Ufungaji wa vifaa vya mfumo wa ufuatiliaji wa maudhui umetoa fursa ya kufanikisha usimamizi mzuri wa vituo vya utangazaji kwa kufuatilia maudhui yanayotolewa na vituo hivyo, ikiwemo redio, televisheni na majukwaa ya mitandaoni.

Mfumo huu pia umepelekea kupunguza urushwaji wa maudhui yasiyofaa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Tume ya Utangazaji.

Kazi hii inafanywa na maofisa wabobezi wa Tume ambao wanafuatilia, kurikodi na kufanya uchambuzi wa kina wa maudhui ya kituo husika sambamba na kuripoti matokeo hasi au chanya yaliyojitokeza.

Aidha, Tume imekuwa ikifanya vikao vya mashauriano na wadau wakiwemo ambao vituo vyao vimekuwa vikikiuka kanuni na miongozo ya Tume hiyo na hivyo kuwafanya waweze kuwajibika ipasavyo na kuimariusha ufanisi.

**Ushirikiano wa TUZ na Wadau**
Tume imeendeleza uhusiano na wadau wake tofauti katika kipindi cha uongozi wa awamu ya nane. Miongoni mwa wadau hao ni taasisi zinazosimamia mawasiliano, wamiliki wa vyombo vya habari na taasisi mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali ambazo zinategemeana sana na Tume ili kuweza kusimamia au kufanikisha majukumu yanayohusu kila upande.

TUZ inafanyakazi pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Katika kufanikisha majukumu yao, vikao vya ushirikiano baina ya pande mbili vimefanyika kwa ufanisi na kuendelea kutoa matokeo chanya.

Miongoni mwa hayo ni kuongezeka kwa usikivu wa masafa kwa vituo vya redio za FM katika maeneo ya Unguja na Dar es Salaam, Pemba na Tanga. Vituo hivyo ambavyo vinarusha matangazo yake kwa njia ya kupokezana baina ya Unguja na Dar es Salaam ni pamoja na Mjini FM Redio, Crown Media, Furaha FM Redio na Wasafi Media

Kwa upande wa Tanzania bara vituo vinavyoendelea kunufaika na mashirikiano haya ni Redio Maria, Redio Imani, Redio Free Africa, TBC na Bongo FM.

Kuimarika kwa uhusiano kati ya TUZ na TCRA kunafuatia kufanyiwa mapitio ya hati ya makubaliano ya taasisi hizi mwaka 2023 ili kuimarisha vyema maeneo ya ushirikiano.

Aidha, wanufaika wa mashirikiano haya ya wanaendelea kufurahia wigo mpana wa kuwa na wasikilizaji wengi katika maeneo wanayosikika sambamba na kuzifikia fursa za matangazo na biashara ambapo hapo awali zilikuwa ni adimu kupatikana.

Kwa upande mwengine, Tume imefanikiwa kuimarisha ushirikiano na wamiliki na watendaji wa vituo vya utangazaji kupitia makongamano na mikutano ya kujadili maendeleo ya sekta ya utangazaji nchini.

Kongamano la Vituo vya Utangazaji la Mei 2025 lenye kaulimbiu “Zingatia Maadili ya Utangazaji, Tulinde Amani na Utulivu wa Nchi Yetu” lilitoa fursa ya kubadilishana uzoefu na kubaini kwa kina changamoto za watoa huduma na kuzipatia ufumbuzi.

Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) ni mdau mkubwa wa Tume hususan katika kipindi cha Uchaguzi Mkuu, uchaguzi mdogo, uchaguzi wa marudio, na kura za maoni kwa nafasi zote za wagombea. ZBC TV kurushwa (kubebwa) na mitandao yote ya usambazaji wa maudhui nchini.

Fursa ya ZBC TV inayomilikiwa na Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) ambacho ni chombo cha habari cha umma kuonekana bila malipo kwa watoa huduma wote waliopo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwezi wa April mwaka 2023 ni miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika awamu hii ya nane.

Hii imewezesha kukipunguzia kituo hicho gharama za kufikisha maudhui yake kwa wateja walioko maeneo mbali mbali nje na ndani ya nchi.

ZBC TV kwa sasa imeweza kuongeza idadi ya watazamaji na matangazo ya biashara huku wananchi wa maeneo mbali mbali wakiendelea kunanufaika kwa kupata ajira na kukuza kipato chao. Awali, vituo vya TBC na Safari Chanel pekee ndivyo vilivyokuwa vikifaidika na fursa hii.

**Ongezeko la usajili wa vituo**

Tume ya Utangazaji ndio taasisi inayosimamia na kutoa leseni za utangazaji wa maudhui Zanzibar kwa vituo vya utangazaji ikiwemo redio, televisheni, na huduma za maudhui mtandaoni.

Kwa awamu ya nane Tume imetoa jumla ya leseni mpya 39 zikiwemo nane kwa vituo vya redio, nane kwa televisheni na 23 kwa wanaorusha maudhui ya mtandaoni. Idadi hii imeongezeka ikilinganishwa na leseni zilizotolewa kabla ya awamu ya nane ambazo zilikuwa ni 67.

Aidha, tume imekuwa ikifanya juhudi ya za makusudi kuwashajiisha na kuelimisha wenye vituo kuhuisha leseni zao kwa wakati muafaka.

Kusajiliwa kwa vituo hivi kumeimarisha heshima ya tasnia ya utangazaji, kuzuia madhara ya kijamii na kujenga uaminifu kwa chombo husika mbele ya hadhira wake. Hali hii huviwezesha vyombo vya utangazaji kupata utambulisho rasmi, kufahamika na wadau na kuwepesisha udhamini.

Katika kongamano maalum la vituo vya utangazaji lililofanyika mwezi Mei 2025,



Tume ya Utangazaji imetoa tuzo kwa vituo bora vya Alfatah Online TV, Spice FM Radio, Radio Jamii Mkoani na Sunet TV ambavyo vilikidhi vigezo vya kuhuisha leseni zao kwa wakati.

# Ziara za ukaguzi vituo vya Utangazaji zaimarisha huduma ya matangazo nchini



Katika shughuli za msingi na kawaida za Tume ya Utangazaji Zanzibar (TUZ) ni kufanya ziara za ukaguzi wa vituo vya utangazaji.

Tume hufanya shughuli hiyo mara nne kwa kila mwaka ili kuona jinsi vyombo vya habari vya utangazaji ilivyovisajili vinavyotii sheria, kanuni, miongozo na taratibu zilizowekwa ili kufanikisha majukumu yao ipasavyo.

Ukaguzi huu pia huwezesha kujadili kwa pamoja maendeleo ya sekta ya utangazaji na uongozi wa vituo, kutathmini ubora na ufanisi wa vifaa na mifumo ya usambazaji wa matangazo, pamoja na kubaini changamoto zinazokwamisha utoaji bora wa huduma na maboresha yatayohitajika.

Kikawaida, zoezi la ukaguzi huhusisha vituo vya redio, televisheni, wasambazaji wa maudhui pamoja na vyombo vinavyorusha maudhui mtandaoni vilivyosajiliwa na kupatiwa leseni.

Ziara hizo zimewezesha vituo kadhaa vya habari kujiimarisha kwa kurekebisha kasoro zinazobainika wakati wa ukaguzi. Jambo hili pia hutoa fursa kwa Tume kujifunza mbinu bora za usimamizi na kuweza kujitathmini ni kwa kiasi gani imeweza kusimamia majukumu yake kwa ufanisi.

**Tukio Maalum: Ukaguzi wa Kituo cha Bomba FM**

Katika kusimamia vyema na ukaribu zaidi sekta ya habari, aliyekuwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Mhe. Tabia Maulid Mwita aliungana na watendaji wa Tume ya Utangazaji Zanzibar katika ukaguzi maalum wa vituo uliofanyika tarehe 10 Disemba, 2024.

Miongoni mwa vituo vilivyokaguliwa kwa siku hiyo ilikuwa ni Bomba FM. Siku hiyo, Mhe. Tabia alikifungia kituo cha redio hiyo kilichokuwepo Kiembesamaki Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja baada ya kutoridhika na mazingira pamoja na miundombinu iliyokuwepo kituoni hapo.


Kituo hicho kilisitishwa kurusha matangazo yake kutokana na changamoto kadhaa zilizobainika katika ukaguzi ikiwemo kiwango kisichoridhisha cha vifaa vya studio ya kurushia matangazo, mazingira mabovu na machafu ya jengo na ukosefu wa choo ambavyo vilichangia kuhatarisha usalama wa wafanyakazi na wageni wanaofika kituoni hapo.

Bomba FM Radio imefanya mabadiliko makubwa na ya haraka ya jengo, kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi, miundombinu ya studio na vifaa kwa mujibu wa muongozo wa Tume ya Utangazaji Zanzibar.
Hali hiyo imekiwezesha kituo hicho kuweza kurejea kutoa huduma za utangazaji ambapo hivi sasa kinaendesha shughuli zake katika mazingira salama katika jengo lake liliopo Shehia ya Chukwani.

**Ziara Bahari FM**

Bahari FM ilikaguliwa katika eneo lake hapo Migombani. Ukaguzi ulibaini uchakavu mkubwa wa miundombinu uliokuwa ukiifanya redio hiyo kutofanyakazi katika kiwango kinachostahiki.

Kama zilivyo taratibu, Tume ilitoa miongozo ya kuboresha mazingira ya sehemu hiyo ya kazi pamoja na miundombinu yake ili kuwepesisha ufanyaji kazi na kukiweka kituo katika mazingira salama zaidi.



Hatua hii ya uimarishwaji wa usalama katika vituo hivi pia imechangia sana kudhibiti hali ya ulinzi na usalama kwa miundombinu ya vifaa vya kurushia matangazo na wafanyakazi.

Awali, Tume ilibaini kuwa baadhi ya studio katika vituo vya redio Alnoor, Zenj FM, AM24, Furaha FM, pamoja na redio jamii ikiwemo Mwenge FM, Kati FM, Habari FM kutokuwa na miundombinu hiyo.

Kwa ujumla ukaguzi wa vituo vya utangazaji ni njia muhimu katika kuimarisha sekta ya utangazaji nchini na ni sahihi kuwa ukaguzi huo umewezesha sana kusaidia kuimarisha viwango vya kitaaluma, maadili ya utangazaji na uzingatiaji wa sheria, kanuni na miongozo ya Tume na kuiwezesha jamii kupata maudhui bora inayoyahitaji.

Kuimarika kwa jengo jipya la kudumu la kituo cha utangazaji cha Bahari FM hapo Migombani, Wilaya ya Mjini ni miongoni mwa matokeo ya ziara za ukaguzi huo.

Kwa sasa Bahari FM iko katika hatua za mwisho za ukarabati unaohusisha studio tatu za kisasa, ofisi za watendaji, ukumbi wa mikutano pamoja na stoo za kuhifadhia mahitaji yao.

**Vituo vya Utangazaji na mabadiliko ya teknolojia**
Ziara za ukaguzi zimewezesha kubaini kuwa yapo maendeleo ya kasi ya teknolojia katika vyombo vya utangazaji ambayo yamepelekea wepesi wa uzalishaji wa maudhui yenye ubora na utaalamu wa hali ya juu sambamba na kurahisisha kazi ya uhariri wa taarifa mbali mbali.

Hali hii inatokana na kuimarika kwa miundombinu ya studio za kisasa zenye kutumia teknolojia inayohusisha kompyuta zenye uwezo mkubwa, vifaa vyenye ubora wa udhibiti wa sauti na picha, sambamba na matumizi ya kasi ya mtandao.

Hili limebainika takriban katika vituo kadhaa vya redio ikiwemo Al Noor Radio, ZBC, Spice FM Radio, Crown FM na Mjini FM. Kwa upande wa televisheni, vituo vilivyoboresha shughuli zake kwa matumizi ya teknolojia ya habari ni pamoja na ZBC TV na SUNET TV.

Ukuaji wa teknolojia ya kidijitali umewafaidisha pia warushaji wa maudhui ya mtandaoni kwa kurusha maudhui kwa kutumia vifaa vya kisasa kupitia majukwaa ya mitandaoni ya kijamii ikiwemo Youtube, Tiktok na Facebook.

**Usalama katika vituo vya utangazaji**
Ukaguzi umeonyesha kuwa vituo vya redio vimekuwa vikiimarisha usalama wake hatua kwa hatua.

Ukaguzi unaoendelea kufanywa umebaini mabadiliko ya kiwango bora zaidi kwa baadhi ya vituo vya utangazaji vikiwemo redio na televisheni ya ZBC, Crown, NRG pamoja na wasambazaji wa maudhui BAYT.

Vituo hivi vimeimarisha kwa kiwango kikubwa usalama kwa kuweka vifaa vya kuzimia moto na mifumo ya kiteknolojia ikiwemo alama za vidole “fingerprint”.

# Wajibu wa Vyombo vya Habari vya Umma katika kuimarisha tasnia ya Utangazaji Zanzibar

Na Yussuf Khamis

Vyombo vya Utangazaji vya Umma (Public Service Broadcasting - PSB) ni mfumo ambao televisheni, mitandao ya kijamii na redio huwa zinahudumia jamii.

Ni mfumo wa utangazaji unaolenga kutoa huduma kwa umma kwa misingi ya maslahi ya kijamii, kiutamaduni, kielimu na kisiasa, bila kutawaliwa na maslahi ya kibiashara au ya kisiasa.

PSB sio lazima imilikiwe na serikali, lakini hupewa uhakika wa kuhudumia jamii na serikali. PSB ni lazima ifanye kazi kwa kufuata mila, silka na desturi za jamii kwa kulinda utamaduni, ina wajibu wa kutoa burudani, taarifa na taaluma kwa jamii pamoja na kulinda mustakbali wa nchi.

Kihistoria, PSB ilianza mwaka 1926 nchini Uingereza. John Reith, Mkurugenzi wa Kampuni ya Utangazaji ya Uingereza (BBC) mwaka 1923-1926 na Mkurugenzi Mkuu wa mwanzo wa Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) mwaka 1926 - 1938, amefafanua kuwa PSB ni tunu ya jamii (public utility) na nyenzo ya kuimarisha ujenzi wa taifa kwa manufaa ya taifa.

Reith, mbele ya Kamati ya Crawford (Crawford Committee) iliyoundwa kwa lengo la kufuatia mwenendo wa mabadiliko ya sekta ya utangazaji nchini Uingereza alisema "huduma hii (PSB) haipaswi kutumika kwa burudani pekee, bali ina jukumu kubwa la kufika katika kila nyumba tunayoishi na kuonyesha mabadiliko makubwa ya kimsimamo ikiwemo mafanikio na changamoto zetu".

Mawazo ya Reith yalikuwa ni kutoa huduma kwa jamii na kuleta mabadiliko makubwa na maendeleo ya wananchi kwa kuwaunganisha bila ya kujali tofauti zao.

Mtazamo wa Reith juu ya PSB ni kutumia jukwaa la utangazaji katika kuunda hoja za wananchi na wanajamii juu ya mabadiliko yakiwemo ya kisiasa ili kuweza kuunda jamii huru kwa misingi ya demokrasia.

Kwa mnasaba huo, PSB ni mfumo wa utangazaji unaoakisi jamii, matatizo ya wananchi na faraja wanayoitaka. Vipindi vinavyotayarishwa lazima vilenge jamii husika na matakwa na maslahi yao kuweza kubainishwa.

Malengo ya PSB na mchango wake kwa Zanzibar

Kwa Zanzibar, taasisi kuu inayohusishwa na PSB ni Shirika la Utangazaji Zanzibar (Zanzibar Broadcasting Corporation -ZBC) lililoanzishwa mwaka 2013 likichukua nafasi ya iliyokuwa Television Zanzibar (TVZ) pamoja na Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ).

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Television Zanzibar (TVZ) mwaka 1974 ikiwa ni kituo cha kwanza cha televisheni ya rangi katika ukanda wa Afrika, Kusini mwa jangwa la Sahara.

Lengo la kuanzishwa kwake ni kuisaidia STZ iliyoanzishwa 1951 kama nyezo ya kusaidia mapambano dhidi ya ujinga, umasikini na maradhi, dhima ambayo imetarajiwa kufikiwa kupitia vipindi vya ELIMU, BURUDANI na TAARIFA (habari) zinazoakisi matakwa ya jamii.

Hivyo, sera kuu ya Uhariri kwa wakati huo ilikuwa ni 'ELIMU KWA TELEVISION.' Sera hii ndio iliyokuwa kiongozi kwa vipindi vyote vilivyokuwa vikitayarishwa na kuongozwa na taasisi hii.

Viongozi, watendaji wakuu wa serikali, chama na taasisi mbali mbali walipatiwa nafasi ya kushiriki katika vipindi vya elimu, na kila mwananchi wa Zanzibar alijiona ni sehemu ya TVZ, kama ilivyo kwa Uingereza na BBC, Ujerumani na DW, China na Xinhua, Japan na NHK, Ufaransa na ORTF ama Norway na NRK.

Kauli za Viongozi wa Zanzibar kuhusu PSB

Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Abeid Amaan Karume, aliliambia Baraza la Mapinduzi mwaka 1971 kuwa malengo na sera ya kuanzishwa kwa TVZ "ni kuhudumia jamii na burudani kwa wananchi wote," akiongeza kuwa hicho "sio chombo cha kikundi cha watu fulani, sio chombo cha kuingiza faida na kuwanufaisha wanasiasa na vikundi vya uongozi au chombo cha kufanya biashara".

Akifungua semina kuhusu umuhimu wa televisheni, Oktoba 4, 1977, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Aboud Jumbe alisema, iwapo vipindi vya elimu kupitia televisheni vitatayarishwa kwa weledi na uhakika zaidi, vitaondosha kabisa changamoto ya elimu na maendeleo katika jamii.

Aliyewahi kuwa Waziri wa Elimu Zanzibar (1977), Seif Shariff Hamad alisema, mpango wa kuanzisha televisheni ya rangi Zanzibar ni mkakati wa kuimarisha elimu kwa wakulima na wafanyakazi nchini huku akitangaza kuwa televisheni hiyo itakuwa kitivo cha elimu sahihi kwa wananchi.

Mwaka 1999, katika maadhimisho ya miaka 25 ya kuanzishwa kwa huduma za televisheni Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dr. Salmin Amour alisema: 'televisheni Zanzibar imechangia katika kuleta mwamko na hamasa kwa wananchi katika ulinzi na urithishaji wa utamaduni, maendeleo ya uchumi, ukuaji wa sayansi na teknolojia pamoja na kuiunganisha Zanzibar katika sehemu kubwa ya dunia."

Katika kufahamu umuhimu wa mabadiliko ya teknolojia katika sekta ya utangazaji wa televisheni, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa awamu ya saba (7) Dk. Ali Mohamed Shein, mwaka 2016 aliidhinisha matumizi ya Dola za Kimarekani milioni mbili (US$2) kwa ajili ya marekebisho makubwa ya studio za televisheni Zanzibar, huku akisisitiza kuwa kwa wale wote wasiokuwa na elimu ya kutosha na wasio na ajira wapatiwe elimu hiyo kupitia vipindi vya mafunzo ya amali.

Katika kipindi cha awali cha kuanzishwa kwa PSB hapa zanzibar, kulikuwa na wataalamu wa kutosha katika fani tofauti zikiwemo ufundi, utayarishaji wa vipindi na hata katika utawala na uendeshaji.

Hazina ya utaalamu iliimarishwa na kuwa ni miongoni mwa vituo bora vya televisheni sio tu katika ukanda wa Afrika Kusini mwa jangwa la Sahara, bali pia katika Afrika na sehemu kubwa ya nchi za Ulimwengu wa Tatu.

Uchunguzi wa tafiti mbali mbali unaonyesha kuwa katika miaka kumi (10) ya awali ya kuanzishwa kwa huduma za televisheni, Zanzibar iliweza kuzalisha asilimia 80 ya vipindi vya maudhui ya ndani ambavyo viliakisi malengo yaliyokusudiwa.

**Wajibu wa vyombo vya habari vya umma**

Vyombo vya Habari vya Umma ZBC vina wajibu mkubwa wa kukuza, kulinda na kuendeleza tasnia ya utangazaji Zanzibar. Miongoni mwa wajibu huo ni pamoja na:

i. Kuimarisha maadili ya Uandishi wa Habari - Kwa Zanzibar, ZBC ina wajibu wa kusimamia maadili ya kitaaluma kwa kupunguza na kurekebisha upotoshaji wa taarifa unaojitokeza kwenye vyombo mbali mbali ikiwemo mitandao ya kijamii.

   Hii inamaanisha kuwa PSB yenyewe inapaswa kuwa chanzo kikuu cha habari zilizopo katika kiwango cha kitaaluma kinachokubalika ikiwemo kuandika habari zilizo sahihi, zenye uwiano, haki na usawa, zisizotegemea upande wowote na zenye maslahi ya umma.

ii. Kukuza utamaduni, lugha na utambulisho wa Mzanzibari: PSB ina jukumu la kuenzi na kuendeleza Kiswahili fasaha na sahihi cha Zanzibar, mila na desturi, sanaa na muziki pamoja na historia ya Unguja na Pemba. PSB hutengeneza na kutangaza maudhui ya asili ambayo husaidia kuilinda Zanzibar dhidi ya athari hasi za utandawazi wa utamaduni.

iii. Kutoa vipindi vya elimu, afya na maendeleo ya jamii: PSB inapaswa kutengeneza vipindi vinavyolenga elimu ya afya (malaria, mama na mtoto, lishe), kukuza uchumi (kilimo, uvuvi, biashara ndogondogo), uhifadhi wa mazingira pamoja na utalii na maendeleo.

iv. Kuwezesha utafiti, ubunifu na maendeleo ya kiteknolojia: PSB zina wajibu wa kuongoza katika kuanzisha teknolojia mpya zikiwemo kupitisha maudhui mtandaoni na kuingia katika utangazaji wa sauti wa kidigitali. Kwa Zanzibar, PSB ina nafasi ya kutoa mafunzo, warsha na ushirikiano na vyuo vikuu mbali mbali. Hii itakuza utaalamu wa waandishi, wapiga picha, wahariri na watayarishaji vipindi.

v. Kuwa jukwaa la mijadala ya umma: PSB ni jukwaa la majadiliano ya sera, tathmini za utendaji wa serikali, maoni ya wananchi na midahalo ya kisiasa. PSB inalazimika kukuza utamaduni wa mjadala wa kitaaluma na unaoheshimu maoni tofauti.

vi. Kulinda na kudumisha amani, umoja na utulivu wa kitaifa: Kwa Zanzibar yenye historia ya mjumuiko wa tamaduni na siasa zenye ushindani, PSB ina jukumu la kutoa habari zenye kuimarisha amani, vipindi vinavyostawisha umoja, na mshikamano wa kijamii, na maudhui yasiyochochea chuki na uhasama miongoni mwa wananchi.

vii. Kuwezesha ushiriki wa wananchi: PSB Zanzibar inahitaji kupokea na kutangaza maoni ya wananchi kwa kuanzisha vipindi shirikishi (call-ins, talk shows), na kutoa nafasi kwa makundi maalum kama wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu.

Kwa muktadha wa Zanzibar, vyombo vya habari vya umma vina wajibu wa kulinda utamaduni wa Mzanzibari, kutoa taarifa za kuaminika, kuendeleza maadili ya kitaaluma, kukuza elimu na maendeleo na kuanzisha ubunifu katika tasnia.

Mambo hayo ni miongoni mwa masharti makuu ya kanuni na miongozo ya utangazaji ambayo imekuwa ikitolewa na Tume ya Utangazaji Zanzibar katika kudhibiti maudhui yasiyokubalika na ambayo hayajengi mustakbali mwema wa nchi na kukuza Tasnia ya habari.

# Ongezeko la vituo vya utangazaji na athari za kimaadili



Na Mwandishi Wetu

Nchi zote duniani zinaongozwa na sheria kwani bila hivyo, zitakuwa kama serikali za mwituni, kila mnyama anaishi kwa kutegemea nguvu zake ili kupata mahitaji ya msingi ikiwemo chakula.

Na kwa muktadha huo, kila jambo na taasisi zinazohusisha wanadamu lazima zitengeneze sheria za kuongoza shughuli zinazowahusu, bila kujali nafasi, cheo au umaarufu wake.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ina taasisi nyingi zilizoko chini ya Wizara mbalimbali. Miongoni mwa hizo, ni Tume ya Utangazaji Zanzibar iliyo chini ya Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo.

Majukumu ya Tume hii iliyoundwa chini ya Sheria namba 7 ya mwaka 1997, ni kusajili na kutoa leseni za huduma za utangazaji kwa vituo vya redio na televisheni hapa Zanzibar pamoja na vya maudhui ya mtandaoni.

Katika utekelezaji wa kazi zake, TUZ ina nyenzo za kisheria ambazo ni Sera ya Utangazaji (2008), Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Namba 7(1997), Kanuni za Utoaji Leseni za Utangazaji (2020), Kanuni za Maudhui ya Mtandaoni (2019) na Kanuni za Huduma za Utangazaji wakati wa Uchaguzi (2025).

**Utangazaji wa kale**

Hadi Mapinduzi ya Januari 12, 1964, Zanzibar ilikuwa na kituo kimoja tu rasmi cha redio ambacho kikiitwa Sauti ya Tanzania Zanzibar. Sauti ya Zanzibar (STZ) ilianzishwa mwaka 1951.

Wananchi wa mikoa yote, mijini na vijijini walitegemea kupata habari na kufahamu matukio mbalimbali yanayotokea nchini na duniani kote kupitia kituo hiki.

Wakati huo, kituo hicho pamoja na Televisheni ya Zanzibar (TVZ) iliyozinduliwa mapema mwaka 1972 viliongozwa kwa misingi ya nidhamu na kulilenga zaidi kuelimisha jamii katika masuala mbalimbali ya maendeleo.

Elimu ya ukulima, uvuvi, ufugaji, ujenzi, uzalishaji viwandani, malezi, utii kwa watoto na vijana, ilipatikana katika vipindi vya redio na televisheni zetu. Na ndio maana kaulimbiu ya TVZ wakati ilipoanza, ilikuwa 'Elimu kwa Televisheni'.

Hakuna kipindi hata kimoja kilichooneshwa au kutangazwa na vyombo hivyo, ambacho mtu asingeweza kukaa ukumbini na mkwe au mtoto wake kutazama kwa pamoja, kwani nidhamu na staha zilizingatiwa kikamilifu.

**Vituo vya Utangazaji binafsi**

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliporuhusu sekta binafsi kuingia katika uwekezaji wa vituo vya utangazaji nchini mwanzoni mwa miaka ya 2000 ilikuwa na nia njema.

Pamoja na kupanua wigo wa njia za upashanaji habari, pia ililenga kutengeneza fursa za ajira kwa wananchi wake hasa kundi la vijana wakiwemo wahitimu wa skuli na vyuo mbalimbali.

Ni faraja kwamba wafanyabiashara waliichangamkia vyema fursa hiyo tukashuhudia vituo vingi vya redio na televisheni vikifunguliwa kila uchao.

Kwa upande mwengine, ujio wa vituo hivyo ulisaidia kuongeza ushindani kati yao na vile vya serikali, hasa katika kubuni vipindi bora vinavyovutia wasikilizaji na watazamaji wengi.

Hata hivyo, inafahamika kuwa kila jambo jipya hata likiwa la maendeleo na manufaa kwa umma, changamoto hazikosekani.

**Ukiukaji maadili**
Kwa bahati mbaya, ruhusa hiyo ilitafsiriwa vibaya na baadhi ya watu, na kuonekana kama tasnia ya habari imevamiwa.

Huenda hali hii imesababishwa na maendeleo makubwa na ya haraka ya teknolojia ulimwenguni, yaliyopelekea dunia kuwa kiganjani kutokana na kuimarika kwa mawasiliano ya mtandao na simu za kisasa.

Sasa simu imetoka kuwa kifaa cha mawasiliano ya mazungumzo pekee, na kuwa kifaa kinachoweza kuwaleta karibu watu walioko umbali wowote.

Kutokana na nyenzo hiyo, mambo mengi yanaweza kufanyika, kwani simu na kompyuta sasa zimekuwa sinema, redio, kumbi za mikutano na majukwaa ya matukio yanayokutanisha mamia ya watu. Lakini wakati wengine wanatumia TEHAMA kwa maendeleo chanya na kuelimishana, wapo wanaodhani huo ni uhuru wa kujifanyia chochote hata kama ni kukashifu watu, jamii na nchi.

Mbaya zaidi, upepo huo sasa umehamia katika vyombo vya habari vya kielektroniki, yaani redio na televisheni.

Pamoja na jitihada kubwa zinazochukuliwa na Tume ya Utangazaji Zanzibar kuwaelekeza wanahabari kufuata sheria na maadili ya kazi zao, bado kutii limekuwa tatizo kwa wengine.

**Vipindi visivyofaa**
Baadhi ya televisheni zimekuwa zikiandaa vipindi vinavyoonesha mambo machafu ambayo si katika utamaduni wa Zanzibar.

Vituo kama hivyo havina utaratibu wa kuzikagua filamu za kigeni zinazoingia nchini, na huzionesha bila kujali muda na rika la watu wanaozifuatilia.

Itakumbukwa kuwa miaka iliyopita, filamu za kigeni kabla hazijaoneshwa sinema, kwanza zilikaguliwa na jopo la wasimamizi wa mila na utamaduni, na iwapo kunakutwa picha zisizofaa, hutakiwa zifutwe ndipo ziruhusiwe kuoneshwa.

Jambo hilo pia lilifanyika kwa wasanii wa muziki hata wa hapa nchini, kuwasilisha nyimbo zao na kusikilizwa maudhui yake ili kuhakikisha hazina lugha chafu.

Inaumiza kuona sasa wasanii wetu wa hapa nchini wa filamu na muziki wanaosema wanakwenda na wakati, ndio waliofurutu ada kutunga sanaa zinazokwenda kinyume na maadili.

# PICHA ZA VYOMBO VYA HABARI

Kwa habati mbaya, katika baadhi ya vyombo vya habari hakuna wasimamizi na wahariri wenye macho ya kuona na kuamua lipi ndilo na lipi halifai kutangazwa.

Redio zinaendeshwa na Ma-DJ wenye kupenda muziki na nyimbo wanaodhani kuwa nyimbo zao zenye maudhui hasi zinazobeba maudhui ya matusi zinampendeza kila mtu.

**Mambo muhimu**
Wanaopewa leseni za utangazaji, wanapaswa kuzingatia ubora wa huduma, kuepuka ukiukwaji wa maadili, na kuhakikisha maudhui yanayopelekwa kwa umma ni sahihi na yenye manufaa.

Si kila sanaa inayopelekwa katika vituo inafaa kutumika, bali kwanza uzingatiwe ubora wake kimaadili.

Tatizo linaloonekana, ni kuweka mbele maslahi ya kifedha, kwa kile kisingizio cha kutokupata matangazo mengi.

Kwa hivyo, fedha imevigeuza vituo vya utangazaji kuwa sawa na jaa kila mwenye taka zake atupe.

**Uchafuzi wa lugha**
Ukiukwaji maadili kwenye vituo vya utangazaji hauishii katika maudhui tu, bali hata lugha adhimu ya Kiswahili imekuwa ikichafuliwa mno.

Watangazaji wengi ambao ni vijana wa kizazi cha sasa, hawaoni au hawajui namna bora ya kutumia maneno.

**Hatua zinazochukuliwa na mamlaka**
Katika hali hii, taasisi zenye dhamana ya kusimamia weledi na maadili ya utangazaji na utamaduni Zanzibar, hazikukaa kimya. Zimekuwa zikitoa elimu kila inapojitokeza haja ya kufanya hivyo, ili kuhakikisha vituo vinabaki kwenye mstari kwa kuzitendea haki leseni zao.

Kumbukumbu zinaonesha kuwa, mwezi Oktoba 2022, Tume ya Utangazaji Zanzibar ilivipiga marufuku vituo vyote vya utangazaji (Redio na TV) na mitandao ya kijamii, kucheza, kupiga, kusambaza mitandaoni wimbo wa 'Malaya Twajuana'.

Wimbo huo uliimbwa na wasanii tofauti wa nje ya Zanzibar akiwemo msanii mmoja wa taarab kutoka Unguja.

Wakati ikichukua hatua hiyo, Tume ilisema miongoni mwa majukumu yake ni kudhibiti na kusimamia shughuli za utangazaji Zanzibar, pamoja na kulinda sera, usalama, mila na utamaduni wa visiwa hivi usiharibiwe.

Ilieleza kuwa, kwa mamlaka iliyopewa kisheria chini ya kifungu cha 16 (e) cha Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Nambari 7 ya 1997, haitasita kuchukua hatua za kisheria kwa kituo chochote cha utangazaji, au mtu atakaekwenda kinyume na matumizi ya leseni.

Kwa mfano miezi ya karibuni, Tume iliwahi kukiandikia kituo kimoja cha televisheni hapa Zanzibar na kukitaka kisitishe kuonesha filamu moja ambayo maudhui yake yakikuza taharuki katika jamii.

**Hitimisho**
Ili kukomesha vitendo vya ukiukaji wa maadili katika vituo vya utangazaji, inashauriwa kuwa wamiliki wanaowekeza kwenye biashara hiyo, wapewe semina za mafunzo ili wajue dhima wanayoibeba.

Aidha wapewe miongozo inayotakiwa kufuatwa na wafanyakazi wanaowaajiri, na wakishindwa wawajibike pamoja nao. Suala la kujuana lisipewe nafasi katika uchukuaji hatua pale sheria zinapovunjwa.

Na kwa kuwa utangazaji ni taaluma, mamlaka zihakikishe fani hiyo haivamiwi na watu ambao hawajaisomea katika vyuo vinavyotambuliwa kisheria.

# Wasemavyo Wadau wa Tume ya Utangazaji



**Bakari Masoud Bakar**
Msimamizi Swahili Online TV

"Ninavyoiona Tume ya Utangazaji Zanzibar, ni taasisi inayojua kazi inayotakiwa kufanya.

Inajali wadau wake ambao ni vituo vya utangazaji bila kuangalia ukubwa au udogo wao, mradi tu kituo kiwe kinatoa maudhui ya kihabari yenye tija.

Mimi binafsi nimewahi kuitwa na TUZ ikaniuliza kuhusu maendeleo ya chombo changu, pamoja na kunishirikisha katika mafunzo mbalimbali ambayo yameniongezea uwezo wa kitaaluma.

Mara ya mwisho ilifanya hivyo katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Nimefurahishwa na hatua ya TUZ kuwaita wamiliki na viongozi wa televisheni na vyombo vyengine vya utangazaji, kuwakumbusha umuhimu wa kufuata sheria, kutoa haki na nafasi sawa kwa vyama vyote vya siasa kurusha vipindi vya kunadi sera na kampeni bila upendeleo.

TUZ haikurupuki kuadhibu, bali huelimisha kwanza na kuvielekeza vyombo visivunje sheria na kukiuka maadili, ikitambua navyo ni sehemu ya ajira kwa jamii hususan vijana.

Ninaishukuru TUZ kwa kuwa karibu na wanahabari wakati huu wakiwa katika mchakato wa kuanzisha Umoja wa 'Online TV' kwa ushauri na miongozo ili kufanikisha jambo hili.

Hii inathibitisha kuwa wasimamizi wetu wanathamini na kujali mchango na msaada wetu kwa nchi katika kuongeza nafasi za ajira.

Hata hivyo, ninaishauri Tume ipunguze kiwango cha malipo ya leseni kwani kwa hivi sasa ni ni kukubwa kwa mazingira ya vyombo vyetu vinavyotegemea matangazo ili kujiendesha, ikizingatiwa kuwa upatikanaji matangazo hayo umekuwa mgumu mno.

Ifahamike kuwa vyombo vya habari binafsi ndivyo vinavyoumia sana na kwamba maisha yao ni ya 'kijungu jiko' sawa na kuku wa kienyeji, utoke ndio ule, na mlo wenyewe ni wa leo kwa leo. Hupati cha kula na cha kuweka akiba.

Naomba sheria iwe makini zaidi kwa wasiokuwa na taaluma kujiingiza katika tasnia ili isiwe kama jaa, kila mwenye taka zake atupie huko. Hao ndio wanaoharibu maadili ya utangazaji.

Sheria iwaangalie kwa makini hawa wanaotumia mitandao kutangaza maudhui yaliyokithiri matusi na taharuki.



**Ali Khatib Dai**
Mkurugenzi Coconut FM

"Tangu ilipoanzishwa, Tume ya Utangazaji Zanzibar imepita katika mikono ya viongozi mbalimbali. Wote wamejitahdi kufanya kazi kwa weledi na kwa kuzingatia sheria na kanuni.

Tunawapongeza wote waliowahi kuongoza Tume hii kwa yote waliyoyafanya kuhakikisha sekta ya utangazaji inapiga hatua ya mafanikio lakini pia inafuata sheria na kusimamia maadili.

Hata hivyo, kwa kuwa sifa ya taasisi ni kuonesha upya kati ya nyakati zilizopo na nyengine, sitakosea nikisema kuwa uongozi wa sasa umeibadilisha sana TUZ katika sura ya ufanisi.

Umeonesha kuwa uongozi si utawala na amri, bali ni kuonesha njia.
Kwa upande huo, pamoja na changamoto kadhaa zitokanazo na utendaji wa vyombo vyetu na kwa Tume yenyewe, uongozi uko karibu na wadau wake, kwa kuturejesha kwenye mstari sisi wenye vituo vya utangazaji pale tunapokengeuka kwa bahati mbaya au kutokujua.

Kwa kujua kuwa vyombo vyetu vinaendeshwa na binadamu wenye sifa ya kukosea au kuwa na upungufu, mkono wa TUZ si mwepesi kukimbilia kufungia na kutoza faini kubwa, bali kuonesha njia.

TUZ haioni tabu kutenga muda wa kukutana na viongozi wa vyombo vyetu au wafanyakazi, kutuelekeza umuhimu wa kuzingatia masharti ya leseni inazotoa, kwa maslahi mapana ya taifa.

Ikitokezea chombo kimepotea, Tume hutumia nafasi yake ya uongozi kusikiliza kabla kutoa maamuzi, na inapolazimika kutoa adhabu, ni kwa sababu njia zote za kukitaka kituo kujirekebisha huwa zimeshindwa bila kuonekana mabadiliko.

Sasa tunafurahia zaidi kufanya kazi na Tume kwa vile imetambua kuwa nasi ni sehemu muhimu kwa maendeleo ya nchi. Tasnia ya habari ni kazi rasmi inayotoa ajira kwa vijana wengi, na kukifungia chombo hakumuumizi mmiliki peke yake, bali mfanyakazi na familia inayomtegemea.

Kwa kuhitimisha, naiomba Tume iangalie upya ukubwa wa malipo ya leseni, ikizingatia kwamba hapa Zanzibar utamaduni wa kulipia matangazo kwa kiwango kinachostahili bado hauungwi mkono ipasavyo na taasisi nyingi.

Hafidh Kassim - Mkurugenzi Mwendeshaji, Zanzibar Cable TV

“PAMOJA na kazi nzuri inayofanywa na Tume ya Utangazaji Zanzibar, ninaishauri iige mfano wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kusimamia maslahi ya taasisi na kuzipunguzia masharti magumu ili ziweze kuishi.

TUZ wanajitahidi lakini bado hawajaturidhisha kwa asilimia kubwa kulingana na mazingira yetu visiwani Zanzibar.

TCRA hawana masharti mengi na magumu kama tuliyonayo sisi, ndio maana televisheni nyingi binafsi zinakufa mapema kwa kukosa kushikwa mkono na taasisi za usimamizi.

Viwango vyao vya malipo ya leseni ni himilivu kwani si vikubwa tofauti na Zanzibar.

Mathalan, bei ya leseni tunayotozwa kwa miaka kumi ya mkupuo ambayo ni shilingi milioni 50 ni kubwa sana.

Huku ni kutudhoofisha kibiashara. Ni vyema TUZ iangalie upya sheria na kanuni zake ili isionekane iko kibiashara.

Tume inapoamua kutengeneza kanuni au hata sheria kuhusu maudhui na vyombo vya habari vilivyo katika dhamana yake, ikae pamoja na wadau ili kupata maoni yao.

Haijuzu kujifungia wenyewe, kuunda kanuni kisha wadau wawe watu wa kupokea tu.

Hali kama hii husababisha ugumu katika utekelezaji wa sheria na kanuni. Jambo hili si zuri kwani nchi inahitaji kodi nasi tunataka ustawi.

Vyenginevyo, TUZ ijue bila sisi taasisi hiyo haitakuwepo; hivyo watuwekee mazingira mazuri kuepusha vifo vya vyombo vya habari, hali itakayoathiri watu wengi wakiwemo vijana tunaowaajiri na familia zao.

Mwarabu Mmadi - Mkurugenzi, KHD Online TV

Kwanza naipongeza Tume ya Utangazaji Zanzibar (TUZ) kwa namna inavyofanya kazi kwa weledi pamoja na ushirikiano inaotoa kwa vyombo vya habari.

Hata hivyo, sisi Online TV tunaiomba Tume itupunguzie kiwango cha malipo ya leseni ambayo kwa mwaka ni shilingi laki tano.

Kwa TV za Online, hiki ni kiasi kikubwa kwani mara nyingi hutegemea matangazo ambayo hatuna uhakika wa kuyapata kwa mujibu wa mahitaji.

Taasisi tunazoziomba ufadhili wa matangazo, zina masharti mengi ambayo wakati mwengine ni magumu kuyatimiza.

Mtu atakwambia kuwa, ili akupe ufadhili lazima ajue habari au chaneli yako inatazamwa na watu wangapi.

Lakini pengine kwa siku unakuta unatazamwa na watu 100 au chini ya hapo, ambao kutokana na ushindani uliopo ni kidogo mno.

Mara nyingi, matangazo tunayopata ni yale yanayowekwa na YouTube, ambayo watazamaji wengi hawayataki.

Mtu akifungua habari na kukuta imetanguliwa na tangazo, haraka analiruka (skip), na akifanya hivyo anatukosesha pesa.

Tumekuwa na kazi kubwa kuwaambia watazamaji wetu wasiyaruke matangazo bali wayaache yamalizike ndipo watazame habari tunazoweka, lakini hawakubali.

Kwa upande mwengine, Tume hutoa mafunzo kwa vituo vya Online TV, lakini wanachukua muda mrefu kufanya hivyo mathalan mara moja kwa mwaka.

Kutokana na mabadiliko yanayotokea haraka ulimwenguni, ni vyema TUZ ione umuhimu wa kutoa mafunzo ya aina mbalimbali kulingana na mahitaji ya wakati uliopo.

Wenzetu Tanzania Bara wanapata mafunzo ya mara kwa mara; kwa mfano kuhusu upigaji picha wa kisasa, tahadhari na mambo mengine.

Mafunzo yasisubiri matukio maalumu kama vile uchaguzi, bali izingatiwe kuwa kila sekta inahitaji maudhui yake kuwasilishwa vyema na kwa nafasi ya kutosha na vyombo vyetu baada ya kupatiwa elimu.

TV zetu zinafikika haraka kwani hata mtu akiwa safarini au nje ya nyumba yake, kazini na maeneo mengine anaweza kutazama na kupata taarifa za matukio yanayotokea nchini na duniani, tofauti na TV za kawaida ambazo hadi mtu awepo kwake au ofisini ndipo aone.

Kwa hivyo, Tume inapaswa kututazama kwa jicho la pekee ili nasi tupate thamani tunayostahiki kwa kuwa sote tunasaidia kuajiri vijana na kuipunguzia mzigo serikali.

Tunahitaji kukua kwa haraka lakini pia kufanya kazi kwa weledi ili kukidhi mahitaji ya soko.

Hili litawezekana iwapo T
kutushika mkono na kubuni
kututoa tulipo na kufika nchi y

# Kibonzo

Tume itazidi
njia mpya za
ya ahadi.

# Spr

ead

# REDIO JAMII MICHEWENI: Kichocheo cha Maendeleo ya Wananchi Kaskazini Pemba

NA HAJI NASSOR, PEMBA

'HII ni Redio Jamii Micheweni, ikikutangazia kupitia masafa ya 97.4 FM. Karibu uwe nasi muda wote, na mimi ni mtangazaji wako, -------------------".

Huu ni utambulisho wa Redio Jamii Micheweni (Sauti ya Micheweni), ikiendelea kuvuma katika anga la Kaskazini, na hasa mashariki ya Pemba kwa zaidi ya miaka 16 sasa tangu ilipoanzishwa mwaka 2010.

Ni redio ya kwanza ya jamii visiwani Zanzibar inayotangaza kwa lahaja maalum ya Kipemba inayotumika zaidi na wakaazi wa Micheweni.

Kituo hiki cha redio ambacho kilipata umaarufu mkubwa kisiwani Pemba kilianzishwa kwa msaada wa Shirika la Umoja wa Mataifa, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo mwaka 2010 kupitia Tume ya Utangazaji Zanzibar (TUZ).

Baada ya msaada wa mitambo na vifaa vya kufanyia kazi kutoka kwa UNESCO, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilibaki na jukumu kubwa la kukilea kituo hicho ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa wanapatikana wafanyakazi wa kudumu wa kukiendesha kituo hicho na hasa watangazaji.

Wakati wa kuanzishwa kwake Redio hiyo iliendeshwa na watangazaji wawili kwa siku ambao walipishana katika kutangaza vipindi vitano pekee. Miongoni mwa vipindi vya awali ni 'asili yangu', 'tubadilike' na 'yaliojiri'.

Mmoja kati ya watangazaji wa mwanzo wa redio hiyo ni Time Khamis Mwinyi anaekiri kuwa mwanzo wa kazi hiyo ulikuwa mgumu.

Time anasema, ufadhili wa UNESCO na matunzo ya Wizara ya Habari wakati huo hayakuacha changamoto. Anasema, kwao changamoto kuu ilikuwa ni utayarishaji wa vipindi.

''Ingawa tulikuwa na mikataba ya kazi, lakini changamoto kuu wakati huo ilikuwa ni jinsi ya kutengeneza vipindi ya kijamii. Jamii ilifuatilia sana vipindi vyetu lakini ujuzi wa kutayarisha vipindi ulikuwa mdogo sana. Kwa kweli tulikosa mafunzo ya msingi ya utangazaji".

Hata hivyo, Time anawakumbuka wafanyakazi wazoefu na mahiri wa iliyokuwa Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ), sasa Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Khadija Kombo na Mchanga Haroub ambao waliwasaidia sana katika kukuza ujuzi wa utangazaji.

"Pamoja na UNESCO kutupatia mafunzo na kutupatia baadhi ya vifaa kwa ajili ya kuandaa vipindi, bado tulihitaji uzoefu na mafunzo ya vitendo ya muda mrefu ambayo yalipatikana kupitia walimu wetu hawa," alisema Time.

Mtangazaji mwingine ni Khamis Faki, anayebainisha kuwa Redio Jamii ilikuwa si kitu kinachofahamika kwa wakaazi wengi wa maeneo inamosikika redio hiyo, hali iliyowafanya baadhi ya wananchi kushangaa au kukataa wanapotakiwa kuhojiwa kwa ajili ya maandalizi ya vipindi vya redio hiyo.

''Wakati tukiwakabili baadhi ya wananchi walikuwa wakitukimbia, hali iliyofanya uandaaji wa vipindi vinavyoishirikisha jamii kama inavyohitajika kitaalamu kuwa mgumu sana," anasema Faki.

Hata hivyo, alikiri kuwa kadri siku zilivyoendelea mwamko wa wananchi ulikuwa, na ushirikianao kuanza kupatikana.

Anakumbuka siku moja wakati anakirusha hewani kipindi cha udhalilishaji, alifikiwa studio na kupongezwa na mwananchi aliejisikia akitoa mawazo yake wakati kipindi hicho kikiendelea.

Hamad Shapandu Mwinyi aliekiongoza kituo hicho kwa mara ya kwanza anasema katika hatua za awali za redio hiyo alilazimika kutumuia uzoefu wake wa kihabari kuingia mitaani na kuandaa vipindi na hatimae kutangaza studio ilimradi shughuli za redio hiyo zisisite.

''Mimi wakati nakabidhiwa redio hii kuwasimamia vijana, nilishakuwa mzoefu katika fani ya habari. Hata hivyo, katika baadhi ya nyakati nililazimika kufanya kazi za kitaalamu katika fani ya habari na utangazaji ili kuhakikisha kuwa matangazo hayasiti na wananchi wanapata habari na taarifa muafaka katika wakati unaohitajika," anasimulia Shapandu.

Kwa kweli tunatoka mbali. Hali ilivyokuwa kabla na sasa hivi ni tofauti sana. Tunashukuru Serikali kwa kutambua haja ya kuimarisha kituo hicho.

Ingawa bado kinatakiwa kijiendeshe, lakini msaada wa serikali umesaidia sana katika kuwepesisha kazi za kituo hicho hadi hivi sasa kikiwa kimeimarika.

Changamoto zaibua faraja: Mafanikio yamejitokeza

Time Khamis amejifunza kuwa safari ya mafanikio huanza na hatua moja, na kwamba changamoto ni sehemu ya mafanikio; huzaa mbinu, maarifa na njia mbadala za kuendeleza matlaba ya mtu.

Wakati baadhi ya wananchi wakigomea kutoa baadhi ya taarifa, bado wao kama wafanyakazi waliendelea na kazi ya kurusha vipindi ambavyo walihisi vinahitajika kwa jamii ya Micheweni ambayo kwa kipindi kirefu ilikuwa nyuma kimaendeleo.

Anasema mwaka 2012, waliwahi kurusha hewani kipindi kinachohusu umuhimu wa chanjo kwa watoto, jambo lililopingwa na wananchi wengi wakiwemo viongozi wa dini.

Hata hivyo, mabadiliko yaliyotokea hatua baada ya hatua kutokana na kurushwa vipindi hivyo mfululizo na kuifanya Wilaya ya Micheweni kuwa mshindi wa kwanza katika kufanikisha zoezi la chanjo kuanzia mwaka 2022.

Hali hiyo ilitokana na kuvuka malengo yaliyowekwa na Wizara ya Afya Pemba, ambapo idadi ya watoto waliokusudiwa kuchanjwa ya 28,543 ilizidi.

Meneja mstaafu Hamad Shapandu anasema, hata suala la ndoa za umri mdogo, Micheweni lilikuwa jambo la kawaida, lakini vipindi vya Redio Jamii vilisaidia sana kubadilisha mawazo ya wanajamii ya kuwaacha watoto wa kike waendelee na masomo hadi alau kiwango cha elimu ya lazima.

Wakati ikitimiza miaka 16 tangu kuanzishwa kwake, radio hiyo inajivunia mafaniko kadhaa, ikiwemo kuwa mshindi wa Redio Bora Tanzania kwa maudhui, kwenye mwaka 2018.

Tunzo nyengine ni ya Mwandishi Bora Tanzania na ya kwanza katika historia iliyotolewa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) kupitia kipengele cha kipindi bora cha kilimo; na tunzo ya MCT ya mwaka 2019, ya Chombo cha habari kinachotengeneza vipindi bora kwa Tanzania.

Aidha, Disemba mwaka 2025, Chama cha wanasheria wanawake Zanzibar (ZAFELA) ilikipa tena ushindi kwa Zanzibar nzima, kituo hicho kwa utengenezaji vipindi bora vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia.

Kwa mujibu wa Meneja Ali Masoud Kombo, Redio Jamii Micheweni, imeshaunganishwa na mashirika kadhaa ya kikanda, ikiwemo 'Radio Tadio'

Radio Tadio ni jukwaa la usambazaji wa habari kutoka redio za kijamii, zilizopo Tanzania Bara na Zanzibar.

Kupitia jukwaa hilo, redio washirika ikiwemo ya Micheweni, huchapisha habari, picha, vipindi na kurusha matangazo ya moja kwa moja.

Kituo cha redio jamii Micheweni, kwa sasa kinaendeshwa na watangaazaji 12 huku matangaazo yake yakianza saa 12:00 asubuhi hadi saa 2:00 usiku, ikiendesha vipindi zaidi ya 35 kwa siku saba.

Kituo hicho kinajikita zaidi na vipindi vya kijamii vikiwemo 'Jamvi la asubuhi' kilichokusanya habari mbali mbali, 'wanawake na uongozi', 'asili yetu', na 'haki za watu wenye ulemavu'.

Meneja wa Redio Jamii kuanzia mwaka 2014 ni Ali Massoud Kombo anaesema kuwa hivi sasa redio hiyo imetanua mbawa zake kwa kuunganishwa na mitandao ya kijamii ikiwemo face book, twiter na blog.

Nyenzo ya taarifa kwa viongozi

Redio Jamii Micheweni imekuwa ni nyenzo ya kufikisha ujumbe na viongozi wakuu wa nchi akiwemo Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, wametumia redio hiyo kuhimiza amani na utulivu Oktoba 6 mwaka 2025 wakati nchi ikilekea katika uchaguzi mkuu.

Mkuu wa wilaya ya Micheweni Khatib Juma Mjaja, anasema amekua akiitumia redio hiyo kama sehemu ya ofisi yake, anapotaka kuzungumza na wananchi.

Kwa mambo mbali mbali ikiwemo taarifa za serikali na zinazofanana na hizo.

Wanufaika wa redio

Hamad Mbwana Hija, anasema kabla ya kufikiwa na redio hiyo, walitegemea zaidi vituo vya redio kama KBC ya Kenya na redio Zanzibar kwa habari na matangazo mengine.

Hata hivyo, kuanzishwa kwa redio kumewanufaisha kwa kurahisisha matangazo ya biashara zao na kupata habari nyingi za nyumbani ambazo zinawahusu zaidi kwa mustakbali wao na vizazi vijavyo.

''Niliwahi kufanyiwa kipindi na redio yetu hii na kuhojiwa juu ya kazi yangu. Baada tu ya kutoka studio nilipigiwa simu na wateja na kuanza nao miamala ya kibiashara,'' anasema.

Wadau wengine waliohojiwa walieleza manufaa mbali mbali ya kituo hicho ikiwemo kutoa taarifa zinazohusu umuhimu wa taaluma kwa watoto wa kike, madhara ya ndoa katika umri mdogo, na vipindi vya uchumi na maendeleo vikiwemo kilimo na uvuvi.

Mchango wa Tume ya Utangazaji na wadau wengine.

Ijapokuwa zipo taasisi kadhaa zinazoshirikiana na Radio Micheweni, Tume ya Utangazaji imekuwa mstari wa mbele katika kuimaarisha shughuli za kituo hicho na hasa katika eneo la mafunzo.

Meneja Ali Massoud Kombo, anasema Tume hiyo imekuwa ikiishirikisha redio hiyo katika kutoa mawazo kwenye kuimarisha mambo mbali mbali yanayotawaliwa na Tume hiyo ikiwemo kanuni za utangazaji, sheria, na miongozo inayohusu shughuli za utangazaji.

Akizungumzia kuhusu kazi za Tume ya Utangazaji Zanzibar, Meneja Ali Massoud anasema ni jambo jema kufanya ufuatiliaji wa maudhui.

''Unajua wapo ambao hawana utaalamu wa kuendesha redio, vipindi na hata matangazo ya mubashara, sasa kama hakuna taasisi inayofuatilia, watu watadhalilishwa sana,''anasema Massoud.

Taasisi nyingine ambazo zinashirikiana na chombo hicho cha habari ni pamoja na UNESCO, Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA-Zanzibar).

''Kama TAMWA Zanzibar, UNESCO, MCT na hata Umoja wa vilabu vya waandishi wa habari Tanzania 'UTPC' wamekuwa na miradi maalum, kwa ajili ya utengenezaji vipindi,' wanatusaidia sana na tunawashukuru kwa kweli,' alisisitiza Massoud.

# Nafasi ya mitandao ya kijamii katika utangazaji

RAMADHAN MAKAME

KIHISTORIA utangazaji wa redio duniani ulianza zaidi ya karne moja iliyopita huku mafanikio yake yakichangiwa na wataalam mbalimbali.

Nuru katika fani ya utangazaji ambayo imepiga hatua kubwa, ilianza kung'ara katika mwaka 1905-1906, kufuatia redio kuanza majaribio rasmi ya utangazaji chini ya uvumbuzi wa mtaalamu wa uhandisi wa mawimbi ya redio Guglielmo Marconi.

Baada ya majaribio hayo kupata ufanisi na matangazo kwenye vituo vya redio kuanza kwenda hewani, jambo jengine lililofanikiwa katika kipindi hicho, ni urushwaji wa matangazo ya biashara ambao ulianza rasmi baina ya 1920 hadi 1923.

Huku dunia ikishuhudia kuvumbuliwa kwa chombo hicho kipya cha mawasiliano, tafiti zilikuwa zikiendelea katika hatua mbalimbali kuvumbua teknolojia ya utangazaji itakayohusisha sauti ya mtangazaji na picha yake. Teknolojia hii ya na utangazaji kwa njia televisheni.

Historia inaonesha mfumo wa kwanza wa televisheni ulianza mwaka 1929, ingawa matangazo ya kwanza ya majaribio ya televisheni yalianza mnamo mwaka 1928. Vladimir Zworykin anachukuliwa kama mwanzilishi wa matangazo ya televisheni hayo.

Redio na televisheni ambayo huitwa vyombo vya jadi (traditional media) vimekuwa na umuhimu wa kipekee kwa ajili ya kupasha habari na taarifa mbalimbali, pamoja na kupitiwa na maendeleo ya tekonolojia katika hatua mbali mbali.

Kwa zaidi ya muongo mmoja sasa, utangazaji umeingia kwenye maendeleo mapya ya kidijitali barani Afrika yanayotokana na matumizi ya intaneti na kuwezesha kutumia mitandao ya kijamii kama nyenzo ya utangazaji.

Sio jambo la kushangaza kumuona mtu anasikiliza ama kutazama habari ili kupata taarifa mbalimbali za redio ama televisheni pamoja na burudani kupitia simu ya mkononi au kompyuta iliyounganishwa na mitandao ya kijamii. Kupitia teknolojia hii, mtu mmoja anaweza kubadilishana taarifa na mwengine kwa urahisi.

Bara la Afrika linakadiriwa kuwa na watumiaji wa simu za mikononi wapatao milioni 520, ambao wana uwezo wa kujiunga na mitandao ya kijamii kama WhatsApp, X, Instagram na TikTok kwa ajili ya kupata habari na taarifa.

Ripoti ya takwimu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) za robo ya tatu (Juni -Septemba) ya mwaka 2025 inabainisha kuwa Watanzania milioni 56.3 wameunganishwa na huduma ya intaneti kufikia Septemba mwaka 2025.

Kutokana na wasikilizaji na watazamaji wengi kugeukia mitandao ya kijamii katika kupata taarifa na habari, vyombo vya habari vya jadi (redio na televisheni), navyo vimeamua kufuata mkondo wa matumizi ya mitandao.

Vituo hivyo vikongwe, navyo vinapakia taarifa kupitia mitandao ya kijamii mara tu wanapozipokea katika vyumba vya habari, hatua ambayo nayo inaviwezesha kwenda na wakati.

Kwa mfano, vituo vya redio na televisheni vilivyopo Zanzibar na nchi nyengine za Afrika vinatumia mitandao ya kijamii kwa

ajili ya kusambaza taarifa kuifikia hadhira kwa haraka zaidi.
Utangazaji katika mitandao ya kijamii umekuwa na faida kadhaa, moja wapo ikiwa ni kuingia kwenye mtandao na kuipata kwa ukamilifu wake taarifa iliyokupita kwa siku, miezi na hata miaka kadhaa.

Faida nyengine imerahisisha zaidi upatikanaji wa habari, taarifa, burudani na matukio, ikilinganishwa na vyombo vya jadi ambavyo huwa na mchakato mrefu wa kuandaa taarifa za habari.

Kuibuka kwa mitandao ya kijamii, kumefungua soko la ajira kwa vijana waliosomea uandishi wa habari, kwani vijana wengi wanamiliki redio na televisheni za mtandaoni ambazo ni rahisi kuziendesha na zimekuwa tegemeo kuwapatia vipato.

Mitandao ya kijamii imeleta usawa katika mtiririko wa taarifa na kuvunja ukiritimba ambao vyombo vya habari vya jadi vimekuwa nao.

Mambo yamekuwa sio tena watazamaji kupokea tu taarifa, bali hadhira nayo imekuwa shirikishi katika kuunda, kusambaza na kuchambua habari.

Mtu yeyote katika umma anaweza sasa kuchangia na kudhibiti habari na kufikia hadhira kwa wakati halisi, mara nyingi kwa kasi zaidi kuliko watangazaji wa jadi wanavyoweza.

Bila kuhitaji tena kuwa “eneo la tukio,” watangazaji sasa wanaweza kutumia maudhui yanayotengenezwa na watumiaji ili kutayarisha habari kwa haraka zaidi na kwa gharama nafuu. Kisha wanaweza kutumia wafuasi wao wengi kusambaza habari kwa hadhira kubwa zaidi.

Pamoja na mitando ya kijamii kuleta mageuzi makubwa kwenye tasnia ya utangazaji, hata hivyo kumejitokeza changamoto nyingi, ikiwa ni pamoja na kutozingatiwa kikamilifu maadili ya uandishi wa habari.

Vyombo vingi vya mitandaoni vimejikuta vikirusha hewani kila kitu bila uchujaji hatua ambayo wakati mwengine imekuwa ikileta taharuki za picha na taarifa zinazopakiwa kwenye vyombo hivyo.

Vituo vya utangazaji wa kwenye mitandao vimeingiliwa na wanaoitwa wanaharakati hasa wa kisiasa, kidini na kidemokrasia, hivyo kuonekana kama vinashiriki kuchochea jamii.

Changamoto zinazoibuka kutokana na maendeleo ya teknolojia ya utangazaji zinalazimisha mabadiliko ya Sheria za Udhibiti wa Shughuli za Mawasiliano na Utangazaji ili kuzuia athari zinazoweza kuleta maafa ya kijamii na mtu mmoja mmoja.

Kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na Tume ya Utangazaji Zanzibar kupitia sheria zake mbali mbali zimeweka kanuni za udhibiti wa Maudhui ya Mtandaoni.

Kanuni hizi zinalazimisha kutimiza vigezo maalum ili kuruhusiwa kutangaza ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa warusha maudhui ya mtandaoni wanasajiliwa rasmi ili waweze kufahamika na kufuatiliwa kama ilivyo kwa vyombo vya jadi.

Ni jambo la busara na lazima kwa kila mmiliki au mtangazaji, awe wa kituo cha utangazaji cha nje au ndani ya mtandao ahakikishe kuwa anafuata taratibu za kisheria zilizowekwa na serikali katika umiliki wa kituo chake cha utangazaji.

Ni vyema pia kuwa makini katika kuutumia uhuru wa kujieleza na kutoa maoni uliobainishwa katika Sheria na matamko mbalimbali kuhakikisha kuwa uhuru huo hauathiri haki ya mwengine ikiwemo ya faragha na kutostahiki kukashifiwa.

# Ukosefu wa weledi wa lugha unavyoathiri ladha ya utangazaji

Na Mohammed Mzee Ali

Wakati huo redio ilikuwa (Tere)
Fani ya utangazaji ni kongwe hapa visiwani. Ilianza mwaka 1951 na ilikuwa ni ya kwanza kwa nchi za Afrika Mashariki.

ikiitwa Sauti ya Unguja kabla ya kubadilishwa jina baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 na kuwa Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ).

Sauti ya Unguja wakati huo ilikuwa na watangazaji mahiri waliofunzwa na wakiwa na weledi mzuri wa lugha ya Kiswahili na utamaduni wake, jambo ambalo lilivutia wasikilizaji na kuwa ni kigezo na kituo cha kupigiwa mfano kwa redio nyengine.

Watangazaji wenye weledi mkubwa waliotambulika kimataifa kwa wakati huo ni pamoja na Ahmed Rajab, Salim Said, Salim Mzee wakifuatiwa na David Wakati, Ahmed Rashad Ali na kadhalika.

Wengine waliofuatia ni Haidar Jabir Al Farsy, Joseph Caitan Asama, Nasra Mohamed Hilal ambao nao walifuatiwa na akina Hassan Vuai Mbarouk, Suleiman Juma Kimea na Mohamed Suleiman (Tall) anaesikika hadi leo akitangaza kwa ufasaha katika kipindi cha Maelezo baada ya Habari (ya kiislamu) cha ZBC Radio.

Watangazaji wote hawa waliwavuta wasikilizaji wengi kwa sauti zao maridhawa, na ndio waliochangia sana kuanza utamaduni wa utangazaji wa Kiswahili kwa ufasaha.

Zama za utamu wa sanaa ya utangazaji hapa Zanzibar inaonekana zimepita na hivi sasa ni tirigivyogo tu. Matangazo ya redio yaliyojaa makosa ya kilugha, kilafudhi, kimatamshi na hata kimaadili yamewafanya baadhi ya wasikilizaji kupoteza hamu ya kuyasikiliza.

Tasnia hii ya Utangazaji hivi sasa imevamiwa na vijana waliokosa uweledi wa lugha ingawa mapenzi yao kwa kwa vipaza sauti ni makubwa mno.

Baadhi ya watangazaji hao hawafahamu kuwa kinachotoka kwenye redio kinakuwa ni cha kuaminika, lakini kwa kwa bahati jamii isiyofahamu inalishwa lugha ya makosa, jambo ambalo ni hatari kwa mustakbali wa utamaduni na lugha ya Taifa.

Makosa ya watangazaji
Makosa yanayofanywa na watangazaji wa Redio na Televisheni ni mengi yakijumuisha yale ya matamshi, kuingiza maneno ya kigeni, uteuzi mbaya wa msamiati pamoja na upatanisho wa kisarufi.

Makosa ya matamshi
Imekuwa ikichukiza unaposikia matamshi mabaya ya kiswahili katika utangazaji yanayoondoa utamu wa lugha ya Kiswahili.

Mathalan, watangazaji wengi hutamka kitamkwa 'za' pahala, pa 'dha', zarau' badala ya 'dharau', 'zambi' pahala pa 'dhambi' na pia 'zahabu' badala ya 'dhahabu'.

Aidha , utawasikia watangazaji wakitamka neno 'zana' badala ya 'dhana' au 'nazani' badala ya 'nadhani' (nafikiria). Mfano utamsikia akisema: "nazani umefika wakati wa kuanza kipindi chetu", badala ya "nadhani umefika wakati wa kuanza kipindi chetu".

Maneno mengine yanayotamkwa sivyo ni yale yenye vitamkwa 'tha', ambapo watangazaji wengi hutamka kwa 'sa'. Kwa mfano utamsikia mtangazaji akitamka neno 'samani' pahala pa 'thamani'. Mfano husema: " chombo hiki kina samani ya shilingi milioni 10," badala ya kusema: "chombo hiki kina thamani ya shilingi milioni 10".

Aidha, katika utamkaji wa tarakimu za hesabu watangazaji wengi hasa wa hizi Redio za FM wakitamka " salasini" badala ya "thalathini" na pia "samanini" pahala pa "thamanini".

Kwa upande mwengine watangazaji hutamka neno 'faraha' badala ya 'faragha'. Wakisema: "alikuwa na mazungumzo ya 'faraha' badala ya kusema "alikuwa na mazungumzo ya faragha".

Mara nyengine, mtangazaji husema: "ifikapo saa tatu tutakuwa na 'hadisi' za watoto". Neno 'hadisi' ni zito sio pahala pake na mtangazaji alipaswa kusema: "ifikapo saa tatu tutakuwa na 'hadithi za watoto".

Uteuzi mbaya wa maneno (msamiati)
Watangazaji wengi wamekuwa na uteuzi mbaya wa maneno na kuyatumia pasipo pahali pake.
Kwa mfano, utamsikia mtangazaji akisema: "mtu huyo alikutwa amelewa kibao". Neno 'kibao' haliendani kabisa na kulewa. Neno sahihi ni 'chakari'. Ingelitosha kusema: "mtu huyo alikutwa amelewa "chakari".

Makosa pia huwepo katika kuyasifia mapambo ya dhahabu. Mathalan baadhi ya watangazaji husema: "Bi harusi amepambwa kwa dhahabu kedekede". Neno 'kedekede' haliendani na dhahabu. Neno sahihi ni "kochokocho". Hivyo sahihi ni kusema: "Bi harusi amepambwa kwa dhahabu kochokocho".

Mara moja nilimsikia mtangazaji wa kipindi cha Mawio cha Redio ZBC akisema: "natumsikilize mwandishi wetu aliyeko Mayugwani kwa 'wagonga vyuma'". Bila shaka mtangazaji si mweledi wa Kiswahili, kwani alipaswa kusema: 'wafua vyuma' au 'wahunzi' badala ya neno alilotumia. Aidha, wapo wanaosema 'muuza dhahabu' badala ya 'sonara', 'fundi kijiko' badala ya 'fundi muashi', au 'fundi mbao' badala ya 'seremala,'na kadhalika.

Makosa ya upatanisho wa kisarufi
Watangazaji pia wamekuwa wakifanya makosa ya upatanisho wa kisarufi kutokana na mpangilio mbaya wa maneno. Hivi sasa imekuwa ni kawaida kuwasikia watangazaji wakisema: 'langu jina' badala ya 'jina langu'.

Katika mfumo wa sarufi ya Kiswahili hakuna sentensi inayoanza kwa kivumishi kama ilivyo kwa 'langu jina', bali huanza kwa nomino na kufuatiwa na kivumishi ili kuwa 'jina langu'.

Baadhi husema: "kuendesha chombo bila leseni ya njia ni 'kinyume na sheria'". Kwa mujibu wa sarufi ya Kiswahili, kusema hivyo si sahihi. Mtangazaji alitakiwa kusema "kuendesha chombo bila leseni ya njia ni kinyume cha sheria".

Watangazaji siku hizi hutamka neno 'haupo' badala ya 'hupo'. Kwa muktadha wa sarufi ya Kiswahili hilo ni kosa. Nimemsikia mtangazaji akisema: "nadhani bado haupo makini". Hiki si Kiswahili fasaha, bali alipaswa kusema: "nadhani bado hupo makini".

Kwa upande wa michezo, imekuwa ni kawaida kusikia: "KMKM na KVZ zimesare". Hii si lugha ya fasaha ya kiutangazaji. Mtangazaji alipaswa kusema: "KMKM na KVZ zimetoka sare".

Leo ni kawaida kumsikia mtangazaji akisema: "Jana kulinyesha mvua kali katika maeneo ya Kusini".

Kikawaida, mvua husifiwa kwa ukubwa au udogo (rasha rasha). Hivyo si sahihi kusema: 'mvua kali' badala yake inapaswa kuwa 'mvua kubwa'. Mtangazaji anapaswa kujua pia kuwa, jua hua kali, mbaamwezi kali na upepo mkali. Hivyo, si sahihi kusema: 'upepo mkubwa'.

Kuingiza kiingereza katika kiswahili
Makosa mengine kwa watangazaji yanakuja katika matumizi ya maneno au misemo ya Kiingereza bila faida wakati ya Kiswahili yapo na ya asili.

Mathalan, hivi sasa watangazaji wanapenda kutumia neno 'mwisho wa siku'. Katika Kiswahili, hakuna neno 'mwisho wa siku'. Neno hili limetafsiriwa kutoka katika lugha ya Kiingereza: 'at the end of the day'. Lakini Kiswahili kina neno lake la asili ambalo ni 'hatimaye', 'mwishowe' au 'tamati yake'. Kuna ulazima gani wa kutumia 'mwisho wa siku?

Katika Kiswahili hakuna neno "anatuboa". Mfano utamsikia mtangazaji kwa fahari kabisa akisema: "alikuwa 'anatuboa' kwa maneno, ngoja sasa tukuletee ngoma. Kituz-------".

Neno 'anatuboa' si la Kiswahili kabisa! Neno la Kiingereza lenye mzizi wa 'bore and boredom' kwa maana ya Kiswahili ni 'kuchosha'. Jee kuna ulazima wa kutumia 'anatuboa'? Sidhani kama mzee wa kimakunduchi, kipemba na kitumbatu anafahamu neno hilo.

Tufanyeje?
Kwa vile athari ya utangazaji usiozingatia weledi wa lugha umekuwa mkubwa katika jamii, kuna mambo kadhaa yanahitaji kuzingatiwa kabla ya mtu kuingizwa katika tasnia ya utangazaji. Baadhi ya hayo ni:

- Kuwe na vigezo maalum vitavyosimamiwa na Tume ya Utangazaji (TUZ) kwa wanaotaka kuwa watangazaji, badala ya kila mmoja kukamata kipaza sauti bila kuzingatia weledi wake wa lugha.
- Kuwe na ufuatiliaji wa watangazaji na anaeonekana kuwa na makosa mengi ya lugha na kimaadili, anyimwe fursa ya kuwa mtangazaji.
- TUZ kwa kushirikiana na Baraza la Kiswahili Zanzibar iwe ndio chombo cha kutoa ithibati ya mtangazaji baada ya kungalia vigezo makhsusi ikiwemo weledi mkubwa wa lugha ya Kiswahili fasaha katika matamshi na utamaduni wa Mswahili.
- Kupunguza vipindi vya porojo na kuandaliwe vipindi vyenye kutumia muongozo (script). Udhaifu wa utangazaji unaonekana sana katika lugha ya mazungumzo ambayo haichujwi wala kukaguliwa na yeyote kabla ya kutangazwa.

# Utangazaji wa Zanzibar na dhana ya 'Isokongwe haivushi'

Na Mwandishi Wetu

Nilikuwa nchini Marekani mwaka 1995 katika ziara ya masomo kwenye vyombo mbali mbali vya habari nchini humo vikiwemo vya utangazaji.

Nilifika Jackson, Mississippi katika kituo cha Mississippi Educational Television (METV), ambapo nilijifunza mengi likiwemo jambo moja ambalo lilinikaa moyoni mwangu hadi leo.

Jambo hilo ni kuwaona wazee wengi wakiwa wanaendelea kufanyakazi katika kituo hicho. Nikawauliza wenyeji wangu, mbona nimeona kundi la wazee wakiwa bado wanafanya kazi hapa?

Niliyoyakuta Mississipi, ndiyo niliyoyakuta, Washington katika Discovery Channel na Voice of America (VoA). Baadae, Huston, Texas katika kituo cha 39KHTV, Jacksonville, Florida katika WPTV na pia Iowa kwa mafunzo ya Uplinking Satellite.

Mwaka 1996, nilipata mafunzo ya Uandishi wa Habari (Utangazaji) nchini Ujerumani katika Chuo cha Kimataifa cha Uandishi wa Habari (IIJB) ambapo nilipata bahati ya kutembelea vituo mbalimbali vya utangazaji nchini humo.

Deutsche Welle (DW) ni miongoni mwa vituo vilivyonipatia mafunzo. Lakini, suala nililouliza nchini Marekani ndio hilo hilo nililouliza katika vituo vya Ujerumani, mbona nimeona kundi la wazee wakiwa bado wanafanyakazi hapa?

Mwaka 1997 nilipata bahati tena ya kuhudhuria mafunzo ya Uandishi na Utangazaji wa Habari nchini Uingereza, chini ya Reuters Foundation, London. Mafunzo haya yalifanikisha kutembelea katika vyombo mbali mbali vya habari nchini Uingereza.

Nilitembelea Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), Bush House, London, baadae Independent Television (ITV), London na kituo cha matangazo cha SkyNews.
Suala nililouliza nchini Marekani na baadae Ujerumani, ndio hilo hilo nikauliza katika vituo vya Uingereza. Mbona nimeona kundi la wazee wakiwa bado wanafanyakazi hapa?

Wakati nikianza mafunzo ya Shahada ya Uzamili (Master Degree) ya Uandishi wa Habari, Cardiff, Uingereza mwaka 1999 nilikuwa 'mgonjwa' wa vipindi na taarifa zinazosomwa na watangazaji 'wazee' wakiwemo - Trevor McDonald (ITV), Nick Robbinson (BBC) na Shaka Ssali (VoA).

Wengine walikuwa Christine Amanpur (CNN), Larry King (CNN), Laura Kussenburg (BBC), John Laws (AUB), Stephen Sucker (BBC), Zeinab Badawi (BBC), Walter Kronkite (CBS News), David Muir (ABC News), Lester Holt (NBC Nighty News), Andersson Cooper (CNN), Jane Hill (BBC), Andrew Marr (BBC), Lyse Doucet (BBC), David Attenborough (BBC).

Wengine walikuwa wabobezi katika uwanja wa mapambano (vita) ambao ni pamoja na John Simpson (BBC), Olivier Weber (FTV), Kenji Nagai (AFP), Terry Lloyd (ITN), Robert Fisk (ITN) na Andrew Beatty (AFP) - Hawa ni wachache kati ya wengi ambao nimekuwa nikiwafuatilia na kujifunza kutoka kwao.

Usuli huu unatokana na majibu niliyoyapata kote nilikowahi kuuliza katika 'msafara' wa masomo yangu hasa nikiwa nje ya nchi. Wengi waliniambia ya kwamba matumizi ya watangazaji na waandishi wazoefu na wabobezi katika kituo cha utangazaji hujenga zaidi uaminifu na kukubalika kwa kituo katika jamii husika.

Kule Mississipi waliwataja wale 'wazee' kuwa ni hazina na kwengine kote nilikopita jibu likawa ni moja tu, ni hazina ambayo haiwezi kutupwa.

"Wengi wanajifunza kutoka kwao, na tunaowatuma nje tunauhakika mkubwa wa kupata kilicho bora na pia kuaminika kwa kituo chetu," Lisa Gardner, Mtawala mkuu wa Discovery Channel, Baltimore, Maryland, alinieleza.

Ravi Gutter kutoka Texas alinieleza kuwa 'wakongwe' hao ni kamusi katika kituo chao, akinitambulisha kwa 'mkongwe' Gomez Francisco, mtayarishaji na mtangazaji wa kipindi cha 'Matukio ya Wiki, Texas.' Kipindi kama hiki kikaanzishwa na iliyokuwa TVZ (na mwandishi wa makala hii, mwaka 1995) kikiitwa 'Zanzibar Wiki Hii' kabla ya kuigwa na vituo vingi vya habari vilivyoanzishwa nchini na katika ukanda wa Afrika ya Mashariki.

Udadisi wa tasnia yangu ya uandishi wa habari, ukanisukuma kuuliza - jee hawa wazee hawana muda wa kustaafu ili kupisha wengine? Wote walinieleza kuwa kustaafu ni suala la lazima katika ajira, lakini sio kila mmoja anapaswa kustaafu muda wake unapofika.

Mwaka 2004 nikiwa DW, Koln, Ujerumani nilizungumza na aliyekuwa Mkuu wa Idhaa ya Kiswahili, Ben Wazir kuhusu suala la kustaafu kwa waandishi wa habari, watayarishaji wa vipindi na watangazaji.
Ben alisema DW wameandaa mpango maalum kwa watangazaji na waandishi wanaomaliza muda wa kawaida wa utumishi.

"Kwa kutambua umuhimu na umahiri wa watangazaji wetu kabla ya muda wa kustaafu kufika huwa tunawaandalia mikataba ya kutaka waendelee. Hii haimaanishi kama hakuna wengine, ila ni kutokana na umahiri wao na kuzoeleka kwa jamii. Wanakuwa wamebeba alama ya kituo chetu," alisema Wazir.

Suala kama hili pia niliwahi kumuuliza aliyewahi kuwa Mkuu wa Idhaa ya Kiswahili, BBC, Tido Mhando ambaye aliweka bayana kuwa 'nguvu ya maji ni mawe.'

Akibainisha kwamba yeye (Tido) alikuwa kiranja cha kutafuta watangazaji wazee na wenye uzoefu wa kutosha kila anapokuwa katika kituo. Alitolea mfano jinsi alivyozunguka na Charles Hillary (sasa marehemu) pamoja na Suzanne Mungy katika vituo mbali mbali alivyowahi kufanya kazi vikiwemo BBC, TBC na Azam Media.

Pia nilizungumza na Hassan Mitawi aliyewahi kuwa Mkurugenzi wa iliyokuwa TVZ na baadae ZBC kwa vipindi tofauti, ambae nae alikiri umuhimu wa wazee kutumika katika tasnia mbali mbali hasa ya Uandishi wa Habari na Utangazaji.

Alisisitiza kuwa kumtayarisha mtangazaji na mwandishi wa habari huchukua muda hadi kufikia kiwango. "Sipingani na matumizi ya vijana katika tasnia yetu, lakini wapi wanatumika? Jee wanamudu katika nafasi wanayoitumikia? Wana uzoefu na upeo wa kutosha katika hiyo nafasi wanayoitumikia?" aliuliza Mitawi.

Hata hivyo, mawazo ya Tido Mhando (BBC), Hassan Mitawi na Ben Waziri (DW), hayapingani kuhusu vijana kupewa nafasi kuweza kuonyesha na kuibua 'vipaji' vyao, lakini wanakiri kuwa vijana ni lazima wapate muda wa kujifunza kutoka kwa 'wazee' kwenye utendaji.

Uandishi, utayarishaji wa vipindi na utangazaji ni taaluma inayohitaji muda wa kujifunza hadi kufikia weledi. Kujifunza kwa vitendo, taaluma, ubunifu (creativity) pamoja na kuipenda kazi yako ni chachu ya kuweza kufikia mafanikio.

Zanzibar ina historia kubwa ya kuwa na waandishi, watayarishaji wa vipindi na watangazaji mahiri wa redio na televisheni, duniani.

Kwa miaka mingi, vituo vingi vya habari na utangazaji vinavyotangaza kwa Kiswahili katika matangazo yao wamekuwa kimbilio

# Tume ya Utangazaji ilivyozima upotofu mitandaoni

Na Mwandishi Wetu

DUNIA iko katika zama za utandawazi uliotawaliwa na mitandao ya kijamii hasa simu za mkononi ambazo zimekuwa jukwaa la kidijitali linaloruhusu watumiaji kuandika, kupokea na kusambaza taarifa mbalimbali zikiwemo picha na video.

Mitandao hiyo imepata umaarufu mkubwa na watumiaji wengi kote duniani ingawa kundi la vijana ndilo linalotajwa kuongoza wakiwemo wanafunzi wa sekondari na vyuo.

Lakini pamoja na faida zake mbalimbali zinazorahisisha maisha, mitandao ina hasara zake pia.

Vijana na maudhui hasi mitandaoni

Miezi kadhaa iliyopita, kuliibuka tabia ovu kwa baadhi ya vijana nchini, kutengeneza maudhui potofu na kuyasambaza kwenye mitandao ya kijamii bila kujali athari zake kwa umma.

Vijana walikuwa wakipita mitaani hasa katika bustani za kupumzikia na kuigiza uandishi wa habari kwa kuwauliza wasichana masuala yanayokiuka mila, silka, utamaduni, maadili ya Zanzibar na taifa kwa jumla.

Wakimaliza kuwahoji hutengeneza video na kuzisambaza katika mitandao, wakidhani wanafanya jambo jema.

Kwa mfano, kijana wa kiume akijiita mwandishi wa habari, akiambatana na mpiga picha, anaweza kumkuta msichana wa miaka 18 au zaidi kidogo amebarizi bustanini na kumshtukiza kwa masuala huku mwenzake akiwarikodi.

Muulizaji: "una mpenzi (boy friend)?
Muulizwaji: "Ndio ninae".

Muulizaji: "Mpigie simu umuambie umemmisi na unamuhitaji kwa jambo fulani (hapa anakusudia faragha)", Msichana atafanya hivyo huku akijidai kuona haya.

Tume ya Utangazaji Zanzibar (TUZ) ndio chombo chenye dhamana ya kusajili vyombo vya habari vya kielektroniki na mitandao ya kijamii vinavyokidhi masharti yaliyowekwa.

Hata hivyo, uchunguzi mdogo uliyofanywa na Tume ulibaini kuwa vitendo vya ukiukaji wa maadili vilivyobainishwa vinafanywa na televisheni za mitandaoni ambazo hazijasajiliwa.

Kauli ya TUZ

Hiji Dadi Shajak ni Katibu Mtendaji wa TUZ ambae anakiri kuwepo kwa mtindo wa kurikodi video mbalimbali na kurusha kwenye mitandao ya kijamii bila kuzingatia taratibu za kisheria na maadili ya Kizanzibari.

Alisema kitu hicho si sahihi kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utangazaji Nam. 7/1997 inayokataza maudhui yasiyozingatia maadili, na ambayo hayana manufaa kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

"Huku ni kuvuka mipaka ya uhuru wa matumizi ya mitandao ya kijamii na si vizuri. Siku hizi kila mtu amekuwa mwandishi anaejipa haki na uhuru wa kurikodi na kurusha chochote atakacho. Wanakosea," alieleza Shajak.

Alisema mambo yanayorushwa hayana tija yoyote kwa jamii, kwani yanachangia kuandaa kizazi kibaya cha kesho.

Katibu Mtendaji huyo alisema Zanzibar na Tanzania kwa jumla zina utamaduni wao uliojengwa kwa msingi ya kukuza kizazi kilicho chema, hivyo si vizuri vijana kutumia uhuru kupita kiasi, kufuata mihemko na kuwa watumwa wa mitandao ya kijamii.

Hata hivyo, alisema wazazi na walezi wanapaswa kubeba dhima ya mabadiliko ya watoto wao katika ulimwengu wa sasa uliojaa athari nyingi hasi kwa vijana.

"Kinachowatoa vijana katika maadili ni uhuru uliopindukia wanaopewa na wazazi, na kuonekana wawe kama wanaishi kwenye ulimwengu wa bata - baba mbele watoto nyuma, si sahihi," alisisitiza Shajak akiongeza kuwa ni jukumu la wazazi kufuatilia kwa karibu vijana wao.

Hatua za TUZ

Tume imechukua hatua ya kusitisha wimbi hilo la upotoshaji wa maadili na matakwa ya tasnia ya habari.

Katibu Shajak anasema kwa kushirikiana na taasisi nyengine ikiwemo Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar (BASSFU) wamepanga mkakati madhubuti kuhakikisha tabia hiyo inakomeshwa katika visiwa vya Zanzibar ikiwemo kutoa elimu ya malezi.

Aliwaasa vijana wasiwe wafuasi wa shetani, na watumie mitandao kwa maendeleo chanya badala ya kubuni mambo yasiyokuwa na tija wala heshima mbele ya jamii wakiwemo wazazi wao.

Mrajis wa TUZ

Ali Hussein Ayoub ni Mrajisi wa Tume ya Utangazaji Zanzibar ambae anasema taasisi hiyo imepewa jukumu la kusimamia mambo yote yanayohusu maudhui ya mtandaoni ambayo yamewekewa kanuni zake.

Alisema kanuni hizo zimeelekeza wazi kwamba ili wapatiwe leseni, watu wote wanaotaka huduma za kusambaza maudhui mitandaoni wanapaswa kwanza wajisajili ili wao na shughuli zao watambulike rasmi pamoja na mahali walipo.

Alifahamisha kuwa, miongoni mwa malengo ya usajili huo ni kuwapa wahusika miongozo na taratibu za namna bora ya kuandaa maudhui yao kabla kuyarusha hewani ili kudhibiti ukiukaji maadili sambamba na kuleta taharuki kwa jamii.

Hata hivyo, alikiri kuwa wengi wa wanaorusha maudhui yasiyofaa, ni wale ambao hawajasajiliwa.

Alisema kanuni za Tume hiyo zimetaja adhabu kwa wanaokiuka taratibu zinazojumuisha faini kuanzia shilingi 1,000,000, kutumikia kifungo au zote mbili.

Aliwashauri wapokeaji maudhui ya habari, sauti au video, wasisambaze, bali waripoti Jeshi la Polisi kwa hatua za kisheria, au wazifute.

Kauli ya BASSFU

Kuhusu tabia hizo, Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU) Juma Chum Juma, alisema kurikodi na kusambaza vitu kama hivyo ni kinyume na mila na silka za Wazanzibari.

Alisema iwe kwa mwandishi aliyesomea mwenye kibali cha kufanya kazi ya habari, au mtu yeyote anayejinasibisha na uandishi, huko ni kuharibu mila na desturi za nchi, ambazo zinatakiwa zilindwe kwa faida ya kizazi cha sasa na baadae.

Alisema si vyema mtu kujifananisha na mwanahabari huku mwengine akikubali kuhojiwa, lakini maudhui wanayooneshwa ni upotofu unaoharibu maadili na kuchafua taswira njema ya Zanzibar.

# Vituo vya utangazaji na changamoto ya uendeshaji wake

Tangu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kuruhusu uwekezaji binafsi katika sekta ya utangazaji, wananchi wengi wamejitokeza kuanzisha vituo vya utangazaji.

Sheria zilizoruhusu

Aidha, Kukua kwa teknolojia kumeruhusu

ITU na baraka ya kuanzishwa kwa -------

Hivi sasa, jumla ya leseni 109 zimetolewa na Tume ya Utangazaji Zanzibar (TUZ) kwa vituo vya Utangazaji vya Unguja na Pemba zikiwemo 11 za Televisheni, 60 za maudhui ya mtandaoni, 32 za vituo vya redio na leseni sita za wasambazaji maudhui. (tofauti katika vipindi tofauti)

Wingi wa mahitaji umesababisha kukosekana kwa masafa ya kurushia matangazo ya FM, baada ya masafa hayo kumaliza.

Wapo ambao wamefanikiwa sana katika kuendesha shughuli zao na wapo wengi pia ambao kiwango cha mafanikio yao si kile walichokitarajia.

Kwa wale ambao hawakufanikiwa ipasavyo, inawezekana ni kwa sababu ya kutofahamu kwa undani juu ya gharama za uanzishwaji wa vituo hivyo na kipato kinachoweza kupatikana na mwekezaji kadri siku zinavyosonga mbele.

Wengi wao walifikiri kuwa kituo cha utangazaji kinaweza kuzalisha fedha nyingi kwa wakati mfupi, bila ya kuzingatia ni mbinu gani zinaweza kusaidia katika upatikanaji wa fedha hizo kutokana na aina ya kituo alichokianzisha.

Matokeo ya hali hiyo ni ima kufa kwa kituo baada ya mwekezaji kushindwa kukiendesha au kulazimishwa kusitishwa huduma kwa kushindwa kulipa ada mbali mbali zinazohitajika kwa ajili ya shughuli hizo.

Ukosefu wa wataalamu wa uhusiano na masoko umevifanya vituo kukosa mbinu za kutafuta wateja wanaohitajika kwa aina ya maudhui ambayo kituo cha utangazaji au mrushaji wa maudhui mtandaoni amekusudia kuwafikishia.

Aidha ukosefu wa mbinu na maarifa ya kutafuta matangazo ambayo ndio chanzo kikuu cha kuendesha kituo cha utangazaji unachangia kukiacha kituo bila mafao ya uhakika.

Hatua muhimu ya kwanza kufikiria wakati mwananchi akitaka kuanzisha kituo cha utangazaji ni kupata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa wataalamu wa fani ya mawasiliano na utangazaji wakiwemo watu ambao tayari wameanzisha vituo vya aina anayoihitaji.

Iwapo ataafiki ushauri katika eneo analohitaji kuwekeza, atalazimika kufika katika vyombo vinavyosimamia shughuli za utangazaji, ambapo kwa hapa Zanzibar ni TUZ, ili kufahamu nini kinahitajika kwao, ikiwemo ada za uanzishwaji na za kila muda zitazopaswa kulipwa.

Uwekezaji katika eneo la utangazaji unahitaji sana ufuataji wa sheria, kanuni na miongozo pamoja na taratibu za kiufundi zinazohakikisha ubora wa matangazo na usalama wa mawasiliano.

Hivyo, ni vyema pia kufahamu mapema ni taasisi ngapi au zipi zinapaswa kufikiwa ili kufanikisha taratibu za uanzishwaji wa kituo.

Kwa hapa Zanzibar, ili kuanzisha kituo cha redio au televisheni, ndani au nje ya mtandao, ni lazima jina la kampuni liwe limesajiliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA), pamoja na kupatiwa leseni na TUZ.

Baada ya kupatiwa leseni, na kuweka miundombinu inayofaa, atahitaji kufikiria aina ya maudhui atayoyarusha ikizingatiwa kuwa vipindi atavyorusha ni lazima viwafiki matakwa ya kitaaluma, maadili ya taifa, sheria na kanuni za mawasiliano na utangazaji.

Hivyo, ufahamu wa gharama za awali ikiwemo leseni na ada za usajili, vifaa vya studio, vifaa vya kurushia matangazo kama vile transmitters, maudhui yatayohitajika, idadi ya wafanyakazi muhimu wataohitajika, sifa zao pamoja na mishahara yao, ni mambo ya msingi sana katika kuanzisha kituo cha utangazaji. Kila moja kati ya matakwa haya ni lazima lifanywe kwa ubora.

Kiutaalamu, ni lazima kufikiria kwa kina namna ya upatikanaji wa maudhui utayoyarusha, kama ni kivutio kikubwa cha hadhira na nyenzo ya matangazo ambayo ni muhimili mkubwa wa kufanikisha shughuli za utangazaji. Ni vyema kujua nani watakuwa ni hadhira wako, na wanahitaji kitu gani.

Kwa upande wa warusha maudhui mtandaoni eneo walipo hadhira si hoja sana kwa sababu kila mtu duniani anaweza kufikiwa na matangazao ya mtandaoni.

Hata hivyo, hoja ni namna gani kituo chako na maudhui yako yanaweza kuwaridhisha watazamaji, wasikilizaji au wafuatiliaji wenye mahitaji, rika, historia na jinsia tofauti.

Kwa vituo vya utangazaji vinavyorusha maudhui nje ya mtandao, hoja ya wapi matangazo yanafika na nani vinampelekea ujumbe ni lazima ifikiriwe na kila mwazilisha wa kituo cha utangazaji.

Hali hii inalazimisha mwekezaji kuwasiliana na TUZ ambayo itampangia masafa yaliyopo katika eneo fulani na kwa wakati maalum.

Iwapo masafa ya kurushia matangazo yatakuwa hayapo, mwenye kutaka kuwekeza atalazimika kuangalia njia mbadala ya kufanya shughuli za utangazaji Sasa mwekezaji anapokosa misingi imara ya utaalamu anajikuta akikwama katikati ya safari, na ili kujinusuru, anachokimbilia haraka zaidi ni kukwepa kulipa kodi na ada za utangazaji za kila muda.

Pamoja na uhalisia wake, malalamiko juu ya ukubwa wa kodi na hatua ya kutolipa kwa wakati kiwango kinachostahiki yanatokana na kukosa mipango madhubuti ya awali na fikra kuwa mara tu mwananchi atapoanzishaa kituo cha utangazaji utaingiza fedha na kupata faida kubwa.

Mawazo hayo yanakuja baada ya kukosa kufikiria mambo yaliyotajwa hapo juu. Baadhi husingizia kuwa Zanzibar ina

wasikilizaji ama wafuatiliaji wachache wa maudhui mtandaoni, hali inayopunguza kiwango cha malipo ya ufuatiliaji. Hoja ni kuwa jee, hili halikuzingatiwa awali?

Kutokana na ukweli kuwa wawekezaji wengi wa vituo vya utangazaji wanaendelea kukiuka taratibu kwa kutolipa ada ipasavyo, TUZ imekuwa ni mipango imara ya kuandaa miundombinu itakayowezesha kukatisha matangazo ya kituo bila ya kukabiliana na mwekezaji au kufika katika kituo cha utangazaji kuhimiza malipo.

Hali hii tayari imefikiwa kwa wasimamizi wengine wa vituo vya utangazaji ikiwemo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Kitu muhimu cha kuzingatia ni kuhakikisha kuwa uwekezaji katika utangazaji unahitaji mipango madhubuti na imara.

Mpango wa biashara si kwa mwekezaji wa bidhaa pekee, bali hata wewe ambae unafikiria kuanzisha kituo cha utangazaji hapo baadae.

# Utangazaji wa Sauti Kidigitali: Teknolojia itakayomaliza changamoto ya masafa ya utangazaji

ISSA S. NYANGA

HABARI katika ulimwengu ni sehemu ya mahitaji ya msingi kwa watu. Hitajio hili ni moja kati ya sababu za msingi za kuvumbuliwa vyombo vya kufikisha taarifa na matukio kama vile redio na televisheni.

Matangazo ya redio kwa kutumia AM (Amplitude Modulation) yalianza rasmi mwanzoni mwa karne ya 20. Teknolojia hii ilianza kwa kusambaza sauti badala ya alama za telegraph zilizotumika hapa kabla.

Baada ya miaka kadhaa, mfumo wa upatikanaji wa matangazo ya redio kwa njia ya AM ulianza kudhoofika taratibu kutokana na kupotea kwa sauti na gharama kubwa za uendeshaji wa mitambo, na hivyo kupelekea kuibuka kwa Utangazaji wa FM uliopata umashuhuri zaidi katika miaka ya 1990.

Kwa wakati huo, teknolojia hii ikiwa na sifa ya ubora wa sauti isiyoweza kuingiliwa kirahisi na mawimbi ya kielektroniki ilipata hadhi na kutambulika katika sehemu kubwa ya dunia.

Mara baada ya hatua hiyo, maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yaliyoambatana na kuibuka kwa vifaa vya kisasa vya mawasiliano kama vile simu na mitandao ya kijamii yalisogeza hatua mpya ya huduma ya utangazaji.

Sasa, utangazaji unafanyika kidigitali zaidi kupitia Teknolojia ya Utangazaji wa Sauti Kidigitali (Digital Sound Broadcasting - DSB).

Hatua hii ya mageuzi ya kiutangazaji ni suluhisho la uhaba wa Masafa ya Utangazaji, changamoto iliyojitokeza baada ya kuanzishwa vituo vingi vya radio FM binafsi na Radio za Kjamii baada ya kuonekana, kwa wakati huo, ni njia bora zaidi ya matangazo yaliyo bora na nafuu.

Hata hivyo, DSB haijafanyakazi Zanzibar. Ili kuhakikisha utangazaji wa redio unaimarika na unaendelea kufanya kazi zake vizuri kwa manufaa ya wamiliki wa vituo, wasikilizaji na Serikali kwa ujumla, Tume ya Utangazaji Zanzibar (TUZ) iko katika mchakato wa kuingiza nchini teknolojia hiyo kama ni hatua muhimu ya kutatua changamoto ya ubora wa matangazo na uhaba wa Masafa ya Utangazaji.

Maana na faida ya DSB

DSB ni mfumo wa kusambaza matangazo ya sauti (redio) kwa kutumia mawimbi ya kidijitali badala ya njia za analojia kama AM na FM.

Mfumo huu huongeza ubora wa sauti, ufanisi wa masafa na uwezo wa kusambaza taarifa za ziada sambamba na sauti. DSB ni neno pana linalojumuisha teknolojia mbali mbali ikiwemo zifuatazo za DAB, DAB+ (Digital Audio Broadcasting), DRM (Digital Radio Mondiale) na HD Radio (IBOC technology).

Licha ya tofauti zao za kiufundi, teknolojia hizi zote zinahudumia kusudio moja, kuongeza ubora na usasa wa utangazaji wa redio.

Mbali ya sauti bora, iliyosafi, isiyovumo, isiyokatikakatika au kupotea kwa mawimbi wakati msikilizaji anapokuwa mbali na kituo cha kurushia matangazo, teknolojia ya DSB inawezesha masafa machache kubeba vituo vingi zaidi zaidi vya utangazaji, hali inayowezesha ongezeko la huduma na kuondoa tatizo la uhaba wa masafa.

Zanzibar inafanya nini kufikia hatua hiyo?

Nchi za Ulaya, Australia na Afrika, zimekubaliana kutumia teknolojia za DAB na DRM kwa ajili ya Utangazaji wa Sauti kidijitali.

Kwa Ulaya na Australia, Utangazaji wa Sauti ya Kidijitali wa DAB/DAB+ upo katika nchi za Ulaya zisizopungua 33. Hata hivyo, kwa upande wa Afrika ikiwemo Tanzania, bado zipo katika maandalizi.

Hivi sasa Tanzania inajiandaa kuteleza DAB+, ambapo hatua na maandalizi ya nyenzo za kisheria, kujenga uelewa kwa

wadau na uwekaji miundombinu katika maeneo yasiyo na huduma za utangazaji zimeanza kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (Tanzania Communications Regulatory Authority - TCRA).

TCRA ni taasisi ya serikali inayosimamia sekta za mawasiliano na utangazaji nchini kutambua umuhimu wa kupanua mawasiliano na ili wananchi wapate redio na TV.

Zanzibar kwa upande wake inasimamia shughuli za utangazaji kupitia Tume ya Utangazaji Zanzibar (TUZ) na tayari imefanya mikutano ya mashauriano na wadau wa utangazaji (watoa huduma na watumiaji) iliyolenga kufikia muafaka wa mfumo wa leseni kwa watoa huduma za Utangazaji wa Dijitali na viwango (standards) stahiki ili kuruhusu uanzishaji wa mfumo huu hapa nchini.

TUZ imekuwa ikitoa ufafanuzi wa jinsi DSB utavyowapa unafuu watoa huduma na watumiaji pamoja na kupokea maoni, mapendekezo na changamoto zinazoibuliwa na wadau kupitia mikutano ya mashauriano.

Katika hatua zinazoendelea, TUZ inaendelea kupitia taarifa za utekelezaji wa mfumo wa DSB kwa nchi mbali mbali huku ikijiandaa kufikisha mapendekezo Serikalini yatakayowezesha mjadala wa namna teknolojia hii mpya itakavyoweza kutumika nchini.

Penye nia pana njia TUZ inaamini kuwa safari ya DAB itafanikiwa hapa nchini kwa kuwashirikisha zaidi watunga sera sambamba na kuweka ukomo wa matumizi ya mfumo wa FM.

Ni wakati muafaka kwa wadau wote kujiandaa kupokea teknolojia hii mpya itakayoifanya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kwenda sambamba na mbadiliko ya dunia katika sekta ya utangazaji.

# Ijue Leseni ya Utangazaji

Leseni ni ruhusa ya mtu au kampuni kufanya kitu ambacho watu au kampuni nyingine hawaruhusiwi kufanya. Leseni ni muhimu katika kuunda mazingira ya utoaji wa huduma yenye udhibiti mzuri, salama, na ushindani ambayo yananufaisha mtoa huduma na umma.

Kikawaida, kabla ya kupatiwa leseni inapaswa mtu kupitia mchakato wa kuangaliwa iwapo sifa na vigezo vilivyoweka vimetimizwa, ikiwemo kulipa ada maalum na wakati mwengine kupewa kipindi maalum cha majaribio kulingana na huduma inayotaka kutolewa. Leseni inaweza kuwa ya muda au ya kudumu.

**Leseni ya Utangazaji ni ipi?**
Leseni ya Utangazaji ni ruhusa au kibali maalum kinachotolewa kwa mtu au shirika ili kutoa huduma za Utangazaji kwa umma kupitia redio na televisheni.

Huduma za Utangazaji zinazokusudiwa hapa zinamaanisha ni huduma za mawasiliano ya redio na televisheni ambayo urushaji wa sauti au picha unakusudiwa kupeleka ujumbe moja kwa moja kwa umma.

Kwa upande wa Zanzibar, tunapozungumza leseni ya Utangazaji tunakususia ni leseni iliyotolewa chini ya masharti ya Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Namba 7 ya mwaka 1997.

Kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha sheria hiyo, ni marufuku kwa mtu yeyote kutoa huduma za utangazaji bila ya kuwa na leseni inayotambulika kisheria.

Tume ya Utangazaji Zanzibar (TUZ) ndiyo yenye dhamana ya kusajili na kutoa leseni kwa vituo vya utangazaji vya redio, televisheni na maudhui ya mtandaoni; sambamba na kusimamia ugawaji wa mawimbi ya Utangazaji kwa wale watoa huduma wanaohitaji kupatiwa mawimbi ya Utangazaji.

**Aina za leseni zinazotolewa na TUZ**

TUZ inatoa leseni za aina nne. Leseni hizo ni:

i. **Leseni ya huduma ya miundombinu ya mtandao (network facility services license)**
Miundombinu ya Mtandao inamaanisha kitu chochote au mchanganyiko wa vitu, vya miundombinu ya uhalisia vinavyotumiwa hasa kwa ajili ya au kwa kuunganishwa na, utoaji wa huduma moja au zaidi za mtandao au usambazaji wa maudhui, lakini bila kujumuisha vifaa vya wateja.

Leseni hii ambayo hutolewa kwa muda usiozidi miaka kumi na inahusu urushaji wa matangazo na utumiaji wa miundombinu, transmita na viunganishi.

ii. **Leseni za huduma ya matumizi (Application Service license)**
Huduma za matumizi inamaanisha utoaji wa huduma za mawasiliano za elektroniki kwa watumiaji wa mwisho kwa kutumia huduma za mtandao zilizo na leseni lakini haijumuishi huduma za maudhui.

Leseni hii inayolipiwa kila baada ya miaka mitano inahusu huduma za sauti, ujumbe, huduma zilizoongezewa thamani na huduma za bahati nasibu zinazotolewa kwa umma.
Hata hivyo, hadi sasa hakuna mtu aliyepatiwa leseni hii.

iii. **Leseni za huduma ya maudhui(Content Service license)**
Huduma ya maudhui inamaanisha huduma zinazotolewa kwa njia ya mazungumzo, au sauti nyengine, data, maandishi au picha, zikiwa za mnato au zinazotembea, isipokuwa pale ambapo zitasafirishwa kwa mawasiliano binafsi.

Leseni hii ya muda wa miaka mitano ipo katika makundi manne kwa matangazo huria (free to air) ambayo ni huduma za utangazaji wa umma, huduma za utangazaji wa biashara, huduma za utangazaji usiokuwa wa biashara na huduma za utangazaji wa jamii.

Aidha, kuna makundi ya leseni za huduma za maudhui kwa huduma za kulipia ambayo ni:

(a) Huduma za Usaidizi (terrestrial) )
(b) Huduma za Usaidizi (satelite)
(c) Utangazaji wa kulipia (terrestrial)
(d) Utangazaji wa kulipia (other technology) na
(e) Utangazaji wa kulipia (cable)

iv. **Leseni ya Maudhui ya Mtandaoni (Online Content Service)**
Maudhui ya mtandaoni" maana yake ni maudhui yanayotangazwa kwa umma kupitia tovuti za intaneti, programu tumizi za kompyuta, majukwaa, blogi, akaunti ya umma, zana za ujumbe mfupi wa papo hapo, matangazo ya moja kwa moja mtandaoni, mikusanyiko na majukwaa mengine yanayohusiana nayo.

Huduma za maudhui ya mtandaoni zinazopewa leseni hii ni redio na Televisheni, na leseni hiyo hudumu kwa muda wa miaka mitano.

**Masharti ya kuomba leseni**
Maombi ya leseni yanawezwa kufanywa na mwombaji yeyote akiwa mtu binafsi, jumuiya, shirika, taasisi ya Serikali au isiyo ya kiserikali mwenye sifa zifuatazo:-

(a) mzanzibari;
(b) kampuni iliyosajiliwa Zanzibar na angalau 51% ya hisa zake zinamilikiwa na Mzanzibari Mkaazi au Mtanzania.
(c) kampuni ambayo haijasajiliwa Zanzibar ambapo asilimia isiyopungua 30% ya hisa inamilikiwa na inainufaisha Serikali ya Zanzibar.

**Masharti ya kutoa huduma za utangazaji**

Mtu yeyote aliyepatiwa leseni ya Utangazaji atalazimika kufuata masharti kadhaa yakiwemo:-

i. Kutokuvunja heshima, kusababisha uhalifu au machafuko ya umma.
ii. Kuwasilisha habari katika vipindi kwa usahihi na bila ya upendeleo.
iii. Kuweka usawa katika vipindi vya dini na kuepuka kushusha

hadhi au kukejeli dini yoyote; kufuja mitazamo, imani au madhehebu ya kidini kwa waumini wa dini au dhehebu fulani.

iv. Kutumia lugha rasmi katika vipindi ambazo ni Kiswahili au Kiingereza.
v. Kuakisi, tamaduni, mienendo, mahitaji na matarajio ya watu katika eneo husika.
vi. Kuzingatia maadili ya taaluma ya uandishi wa habari.

**Nini atafanya mwombaji wa Leseni?**

Mwombaji wa leseni atalazimika kujaza fomu ya maombi ya leseni inayotolewa Tume kwa utaratibu uliolezwa chini ya Kifungu cha 12(1) cha Sheria na kuambatanisha taarifa zifuatazo wakati wa kuerejesha fomu hizo.

i. Cheti cha Usajili wa Taasisi au Biashara;
ii. Mpango wa biashara kwa huduma zinazopendekezwa;
iii. Mapendekezo ya kiufundi, mfumo wa mtandao, na mpangilio wa huduma inayotarajiwa kutolewa ikiwemo mpango wa kusambaza huduma husika;
iv. Maelezo ya kiufundi na muongozo wa matumizi ya vifaa vitakavyotumika;
v. Aina ya bidhaa na huduma zitakazotolewa;
vi. Hati ya makubaliano inayoeleza muundo wa hisa;
vii. Uthibitisho wa uwezo wa kifedha wa muombaji; na
viii. Taarifa nyingine yoyote ambayo Mamlaka inaweza kuhitaji.

**Utaratibu wa kupokea maombi ya leseni**

Muombaji yeyote wa leseni atawasilisha maombi yake TUZ Zanzibar kwa njia ya mtandao, na pale ambapo itatokea hitilafu ya kimtandao, muombaji anaweza kuwasilisha maombi yake kwa njia ya barua pepe info@tuz.go.tz au katika ofisi ya Tume zilizopo Kilimani, mjini Zanzibar.